

# KAMA TAI ATAHARIKISHAVYO



Na tuendelee kusimama kidogo tu kwa ajili ya maombi.

<sup>2</sup> Mikutano hii yote ya mwisho, daima hunikera. Kwa namna fulani, tunapoonana na kuanza kufahamiana, mbona, na kuanza tu kufanya ushirika, basi ni wakati wa kwenda mahali pengine. Sikuzote hunipa hisia ya huzuni. Ila nikiangalia mbele, ninaitazamia siku ile ambayo sote tutakutana tena, na tutakuwa mahali pamoja, labda, kama Yesu akija kabla hatujakutana duniani tena, ambapo kamwe, kamwe hatutaachana.

<sup>3</sup> Sijui ni wangapi wangependa kukumbukwa kwa Mungu, alasiri ya leo, tunapoinua mikono yetu kwa maombi? Bwana awabariki.

Na tuinamishe vichwa vyetu kwa dakika moja tu.

<sup>4</sup> Mwenyezi Mungu, Muumba wa mbingu na nchi, na Mwanzilishi wa Uzima wa milele, na Mpaji wa kila kipawa chema, tunakuja katika vivuli vya rehema Zako, kwa maombi, kwa Jina la Yesu, Mwanao, kukutolea shukrani zetu kwa ajili ya mkutano huu mkubwa wa Tulsa, kwa kile umemaanisha kwetu, mahali fulani mioyoni mwetu ambapo kamwe hatutawasahau watu hawa wazuri. Japo, Roho Wako Mtakatifu akiwa ndani yao, umekuwa ni ushirika wa jinsi gani: mguso mdogo wa Mbinguni maishani mwetu, ujuzi ambao kamwe hatutausahau. Tunaomba, Baba, kwamba Roho Wako daima atabaki ndani ya watu hawa. Jalia, kutoka kwenye kiini cha kusanyiko hili dogo, lisababishe uamsho kuzuka katika kila kanisa nchini kote. Jalia ishara kuu na maajabu zifanikishwe. Tunaomba, Bwana, kwamba utatujalia mambo haya.

<sup>5</sup> Hapa kwenye dawati hili, alasiri ya leo, zimewekwa lesu na vipande vidogo vya vitambaa ambavyo vinawaendea wagonjwa na wanaoteseka. Mungu Mwenyezi, ninakuomba, katika Jina la Yesu, kwamba yeyote atakayeguswa na hizi, aliye mgonjwa, naomba wapone; sio ombi langu mwenyewe tu, Baba, bali ni maombi ya ukumbi huu mkubwa uliojaa Wakristo, alasiri ya leo. Tunayatoa kwa nia moja, kwa wale walio wahitaji.

<sup>6</sup> Bwana, tunaomba kwamba utubariki katika shughuli zingine za leo hii. Tunayaombea makanisa, usiku wa leo. Jalia kuwe na utukufu na furaha isiyoneneka katika kila kanisa. Tupe umwagikaji mkuu wa Uwepo Wako, alasiri hii. Roho Mtakatifu na aingie ndani ya Neno, nalo Neno na liingie ndani ya miili yetu na kukaa hapa pamoja nasi alasiri ya leo. Kwa kuwa tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

Mwaweza kuketi.

<sup>7</sup> Kwa kila mhudumu, kwa wafanyakazi wote, mlinzi, na kwa mabawabu, na wote; kwangu mimi na kikosi changu: Ndugu David, Ndugu Roy, Billy Paul, Loyce, Ndugu Fred Sothmann, Ndugu Jim Maguire, Ndugu Gene, na Leo, sisi sote tunataka kuwashukuru nyote kwa wema wenu, na yale mmemaanisha kwetu katika mkutano huu. Bila shaka mmekuwa wazuri sana. Heshima na upendo kama huo ambao tumekusanya mioyoni mwetu, kwa ajili yenu, kamwe haitafutiliwa mbali. Haifutiki. Nasi tunaamini kwamba Mungu atawapa mambo ya ajabu mmo hata kuliko yote mngeweza kuyawaza ama kuyaomba. Mungu na awape hayo katika utajiri ulio mkuu sana wa neema ya Mwanawe, Yesu Kristo.

<sup>8</sup> Ndugu Tommy Osborn, yuko hapa mkutanoni. Bwana Mungu awe na Ndugu Tommy. Ndugu Oral alianza alasiri ya leo, nami nafikiri mshipa ulitenguka ama kitu fulani, ukalegea, mguuni mwake; basi mara ibada itakapoisha, niko njiani kwenda kumwomba. Na sasa kwa wafanyakazi wote wa Ndugu Roberts na wafanyakazi wa Ndugu Tommy, na kwa makanisa yote na kadhalika: Mungu awe pamoja nanyi, ndilo ombi langu. Si—sikuzote mtakuwa moyoni mwangu, kwa ajili ya wakati huu. Nao Tulsa na usimame kwa muda mrefu, kazi ya Mungu na ibaki ndani yake kwa muda mrefu, ndilo ombi letu. Nasi tunatarajia kurudi tena wakati mwingine pamoja nanyi.

<sup>9</sup> Na laiti tungeweza kuwa wa fadhili kwenu, kwa njia yoyote! Nilizoea kutoa tamshi hili: usiku hauingii giza kupita kiasi, wala mvua hainyeshi kwa nguvu kupita kiasi, ila ambayo tungeweza kufanya lolote lililo katika uwezo wetu kufanya maisha yawe na raha zaidi kidogo na yenye baraka kwenu. Kama tunaweza kuwa msaada wowote kwenu, tujulisheni tu. Tupigieni simu tu huko Jeffersonville, Indiana, BUtler 2-1519, au unipigie tu simu huko Jeffersonville. [Nambari ya simu imebadilishwa—Mh.] Tunaweza kukutumia kitambaa cha maombi, kukuomba, chochote tu tuwezacho kufanya. Sisi ni watumishi wenu katika Bwana.

<sup>10</sup> Kwa hiyo kidogo ni vibaya kufikia mwisho wa ibada kama hii, wakati mlikuwa na wakati mzuri sana hivyo, lakini wakati mwingine hatuna budi kwenda, hata hivyo.

<sup>11</sup> Tukijua hili, ya kwamba ng'ambo tu ya ule Mto, siku moja wakati maisha yamekwisha kabisa, nami niketi kwenye ile meza kuu, itatandazwa kote angani, ile Karamu ya Arusi, nasi tutatazamana mezani, tutakumbuka nyakati hizi huku Oakland. Hapana shaka, huenda chozi dogo likatiririka shavuni mwetu, kwa furaha, naye Mfalme, katika uzuri Wake wote, atatokea, katika joho Lake jeupe la kupendeza, ayafute machozi yote kutoka machoni mwetu, na kusema, "Msilie tena. Yote yamekwisha sasa. Ingieni katika furaha za Bwana ambazo zilitayarishwa kwa ajili yenu tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu." Hiyo ndiyo saa ninayoishia.

<sup>12</sup> Ninaangalia kote chini kwenye wahudumu wanaoshirikiana hapa, na kuona wengi wao walio na umri mkubwa kuliko wangu. Labda hapa nje mtaani, wakiwa na gitaa na tari, wakiitengeneza njia, wakiyatandaza mawe na kulainisha mahali panapoparuza, kusudi huduma hii ambayo Bwana amenipa, iweze kuendeshwa vizuri barabarani.

<sup>13</sup> Ndugu zangu wa thamani, ninajisikia duni, kusimama hapa juu nanyi hapo chini. Hiyo ni kweli. Endapo kuna heshima yoyote itakayotolewa, inawaendea ninyi. Mungu na awabariki sana daima. Siku hiyo wakati thawabu inatolewa, natumaini nitakuwako wakati nitakapowaona mmevikwa Utukufu Wake.

<sup>14</sup> Dakika chache zilizopita, nilikuwa nikiongea na mhudumu mmoja huko nyuma. Jina lake ni Ndugu Nathan, akasema. Anafanya kazi miongoni mwa Wayahudi. Naye akasema, "Ndugu Branham, usiku wa kwanza, wakati ulipokuwa hapa..." Yeye na mkewe. Mke alikuwa mgonjwa. Akasema, "Uliita, huko katika mkutano, na kuniambia mimi ni nani, na kuhusu mke wangu na ugonjwa wake." Kasema, "Amekuwa akipata nafuu, tangu wakati huo, anaendelea vizuri tu." Na barua nyingi nzuri na shuhuda!

<sup>15</sup> Sasa, labda hukuleta leso yako hapa ndani. Kama tunaweza kukusaidia, kwa njia yoyote, kukutumia kitambaa kidogo, sasa, kutakuwa na fomu ndogo. Tuna ratiba ya maombi inayoenda kote ulimwenguni. Watu huamka, saa zote usiku kucha, na kufuata ratiba hii ya maombi. Sikuzote kwenye Mfumo wa saa za Kimashariki, tunaomba saa tatu asubuhi, saa sita, na saa tisa. Hizo ni saa za kutoa dhabihu za Agano la kale la Kiyahudi. Nasi tunaomba hivyo. Na watu kote ulimwenguni huamka kwa nyakati tofauti, katika mfululizo mkubwa wa maombi, ambapo sote huomba pamoja, sisi kwa sisi. Kwa hiyo nina hakika Mungu atasikia maombi. Mambo ya ajabu kama hayo huingia, ambayo amefanya. Nasi tunataka kukuweka kwenye ratiba yetu ya maombi, upate kuomba pamoja nasi kwenye saa hizo.

<sup>16</sup> Na sasa, hapana shaka, ila hivi karibuni sana, nitakuwa kwenye nchi za ng'ambo tena, Bwana akipenda.

<sup>17</sup> Tunakusanya fedha kidogo hapa. Na jambo lingine, Bwana amenifanya kusema hivyo ili niweze kukumbuka. Wamechukua matoleo mawili ya upendo, ninaamini, kwa ajili yangu. Mnajua jinsi ninavyothamini hilo. Sasa, si hata senti moja itakayokwenda kwangu binafsi. Inakwenda kwenye wakfu wa kanisa kwa madhumuni ya misheni za nchi za ng'ambo. Mnaona? Nasi tutafanya vizuri sana tuwezavyo, kuhakikisha kwamba pesa hizo zinawaendea watu wasioweza kuisikia Injili, wasioweza kuja. Na tutafanya vizuri tuwezavyo. Mungu awabariki sana daima, ndilo ombi langu aminifu.

<sup>18</sup> Na sasa, ikiwa unataka moja ya vitambaa hivi vya maombi, niandikie tu. Na ni Sanduku la Posta 325 tu, au Jeffersonville

tu, Indiana, itanifikia. Na ikiwa unataka kukiweka katika Biblia yako, kiweke kwenye Matendo 19. Na watu wengi sana wameniambia.

<sup>19</sup> Mama mmoja alisema, naamini, mwanawe alikuwa amekanyagwa na gari, naye alikuwa akitokwa na damu vibaya sana, kutokana na jeraha kutokana na kioo, na kwa hivyo akakimbia mbio na kuchukua utepe huu. Alikuwa katika... aliishi bara. Naye akaweka huo utepe mdogo juu ya huyo mvulana, ndipo damu ikakoma mara moja. Na vitu vingi kama hivyo.

<sup>20</sup> Mwanamke huko Ujerumani, aliyepooza. Inakwambia la kufanya; kusanya majirani wako Wakristo, wakati vitambaa hivi vimewekwa juu yako, juu ya moyo wako. Naye akasema, baada ya kila kitu kufanywa kama vile tu ilivyokuwa... Alikuwa amepooza kwa miaka kadhaa. Naye akasema, alipotimiza hayo, alisema, "Shetani, sasa huna nafasi zaidi kwa kitu kingine chochote. Ondoka kwangu." Akanyanyuka kitini akaenda zake.

<sup>21</sup> Hiyo ni rahisi tu hivyo. Unaona? Kwa hivyo ikiwa ungetaka kimoja, hakina gharama, hakina malipo. Tuma tu, nasi tutakituma moja kwa moja kwako, kwa barua. Sasa, utapata ka—karatasi iliyorudufiwa juu ya jinsi ya kukitumia. Lakini, kumbuka, nimeomba, mimi mwenyewe, kibinafsi, juu ya—juu ya kitambaa utakachotumiwa. Kama mtoto wangu mchanga alikuwa anaumwa, mke wangu, au baba na mama yangu, nami nilikuwa na matumaini katika maombi ya mtu fulani, nisingetaka iwe ni sala ya katibu. Ningetaka waiombee. "Basi watendee wengine kama unavyotaka wengine wakutendee," kanuni ya msingi. Kwa hivyo, sisi, hakika tutafurahi kukusaidia kwa njia yoyote tuwezayo. Mungu awabariki daima.

<sup>22</sup> Na kila kitu ambacho kimefanywa kimefanywa kwa wema na upendo, nasi tunathamini hilo sana.

<sup>23</sup> Sasa, nikiwa katika nchi za ng'ambo, sikuzote ni vigumu. Kwa sababu, wachawi na walozi, hawaogopi kukushambulia. Hapa hivi majuzi tu, mahali fulani, kulikuwako na yapata wachawi kumi na watano kila upande, wakitoa maneno ya kunuizia uchawi, wakasema wangeita dhoruba na ingenipulizia mbali. Na, amini usiamini, dhoruba ilikuja. Karibu watu elfu thelathini, na mahali hapo pakitetemeka kwa nguvu sana.

<sup>24</sup> Ndugu Arganbright, wa Wafanyabiashara Wakristo, ninyi ndugu mnamfahamu. Alikuwa ameketi nyuma yangu. Akasema, "Ndugu Branham."

<sup>25</sup> Nikasema, "Keti kimya tu. Roho Mtakatifu alinituma hapa." Hiyo ndiyo sababu siendi mahali popote isipokuwa anitume kwanza, ndipo ninajua naweza kuja kwa Jina la Bwana. Mnaona? Nikasema, "Alinituma hapa."

<sup>26</sup> Walikuwa na mahali pakubwa mno palipojengwa, ambapo wako tu na kama mbili kwa nne, na turubai imepigiliwa

juu yake. Basi mahali hapo palikuwa pakiinuka tu juu chini. Papo hapo katika... yapata saa nane alasiri. Paangavu tu palivyoweza kuwa, nayo dhoruba hiyo ikaja katika dakika thelathini. Nami nikasimama tu. Nikasema, “Sio lazima utafsiri haya.” Unahisi nguvu hizo chafu kutoka pande zote mbili. Nao wameketi pale, wakiipindua mikono yao pamoja na unyoya uliokatwa, kwa makasi. Mnajua wafanyavyo.

<sup>27</sup> Nikasema, “Bwana Mungu, Muumba wa mbingu na nchi, Wewe Ndiwe uliyenituma hapa. Unawajibikia huduma ninayoendeleza kwa ajili Yako. Ninaikemea dhoruba hiyo, katika Jina la Bwana Yesu.”

<sup>28</sup> Ndipo ikagawanyika na kurudi nyuma moja kwa moja. Ngurumo zikanguruma zikaondoka, nalo jua lilikuwa likiwaka, chini ya dakika mbili, papo hapo chini. Ndipo maelfu wakakimbilia madhabahuni, na wenye mtazamo wa kikomunisti na kadhalika. Na jinsi. . .

<sup>29</sup> Siwezi kusimama hapa na kuwaambia shuhuda, kwa sababu ni katika mkutano wangu mwenyewe. Ingekuwa bora kama wengine watafanya hivyo. Lakini, maktaba, ningesema kungekuwako na ensaiklopedia, kungeweza kuwa na vitabu vingi sana vilivyoandikwa, ambapo nimemwona Bwana Yesu akifanya katika maskini huduma yangu mwenyewe. Unafikiri ingekuwa kwa watu kama Ndugu Tommy Osborn, Ndugu Oral Roberts? Ni mkuu. Bwana wetu ni mkuu. Hakika ndivyo alivyo.

<sup>30</sup> Sasa ninataka kusoma Maandiko fulani, alasiri ya leo. Nami nina sehemu chache zilizoandikwa hapa, endapo nitazifikia. Halafu tunaninii. . . Ninaamini mwanangu aliniambia kwamba alisambaza kadi za maombi, na tutawaombea wagonjwa.

<sup>31</sup> Iwapo sitamwona yeyote wenu nyote tena, iwapo sitawaona katika maisha haya; nitakapokutana nanyi kwenye Lango lile, kabla hatujaingia kusimama mbele za Kristo, hayo maono kutoka kwa Mungu ni ya kweli na ni halisi. Malaika wa Bwana, na ile Nguzo ya Moto na Nuru, basi nisaidie, Mungu Mwenyezi, Hakim wangu, Yupo. Ni kweli. Naam. Ili mpate kujua kwamba ni—ni kweli. Mungu ni wa kweli. Hawezi kuwa wa uongo na awe Mungu. Yeye ni mwo-. . . Hawezi kuwa mwongo, maana Yeye hana budi kuwa halisi. Iwapo chochote ni cha uwongo, ni Shetani. Lakini Nuru hiyo, nimeiona, nikaiangalia. Na kwangu mimi. . . Naomba mnisamehe ikiwa ninatenda kwa kukufuru, lakini, kwangu mimi, ni Nguzo ile ile ya Moto iliyowafuata wana wa Israeli.

<sup>32</sup> Kwa sababu, ilikaa katika Mtu anayeitwa Yesu, ambaye alikuwa Mwana wa Mungu, na maisha aliyishi yanatolewa tena leo hii na kitu kile kile. Alisema, “Nalitoka kwa Mungu. Nakwenda kwa Mungu.” Sote tunalijua hilo. “Nalitoka kwa Mungu, na ninakwenda kwa Mungu.” Alisema, “MIMI NIKO ambaye NIKO.” Hiyo ilikuwa ni ile Nguzo ya Moto. Hiyo ilikuwa

ni yule Malaika aliyekuwa kwenye kile kichaka. Ilifanyika mwili na kukaa miongoni mwetu; ikarudi tena. Nayo iko katika mfano ule ule leo hii. Mlijua hilo?

<sup>33</sup> Vema, unasema, “Yesu alikuwa...” Naam, ni—ninazungumza juu ya Mungu, aliyekuwa ndani ya Yesu.

<sup>34</sup> Wakati Paulo alipokuwa akienda zake Dameski, Nuru ilimpiga ikamwangusha, Nguzo ya Moto. Hakuna mmoja wa hao wengine aliyeiona, ila Paulo aliiona. Ilikuwa kuu sana hata ikampofusha. Ndipo akasema, “U nani Wewe, Bwana?”

<sup>35</sup> Akasema, “Mimi ni Yesu.” Alikuwa amerudi kwa Mungu, alikotoka.

<sup>36</sup> Kwangu mimi, ni Yeye tena leo, akimalizia kazi Zake ndani yetu, Kanisa, katika siku za mwisho.

<sup>37</sup> Hebu tufungue Kumbukumbu la Torati 32:11, kwa msingi kidogo wa somo. Nasi tutajaribu kufanya mstari wa maombi, kisha tuondoke katika saa moja, ikiwezekana. [Dada mmoja anatoa himizo—Mh.]

<sup>38</sup> Ee Baba Mungu, jinsi kwa unyenyekevu moyoni mwangu ninavyokubali hilo. Iongoze miguu yangu, ushike mkono wangu, Bwana. Jalia kamwe nisiwe kikwazo kwa yeyote, lakini naomba niwe jiwe la kukanyagia kwa kila msafiri anayesafiri. Lijalie, Bwana. Jalia kamwe nisifanye lolote maishani mwangu ambalo lingeweka kivuli juu ya Jina Lako, au kwa huduma Yako. Nami nitafanya yote niwezayo kukutumikia. Ninakushukuru kwa ajili ya hili, katika Jina la Mwanao, Yesu Kristo, Bwana wangu. Amina.

<sup>39</sup> Jinsi hilo linavyounyenyekeza moyo wangu! Kumbukumbu la Torati 32:11:

*Mfano wa . . .*

[Dada mmoja anatoa himizo—Mh.] Amina. [Dada mwingine anatoa himizo.] Amina. Jina la Bwana libarikiwe. [Dada mwingine anatoa himizo.] Jinsi tunavyomshukuru Bwana, kuwa na Roho Wake akifanya kazi miongoni mwetu, katikati yetu.

*Mfano wa tai ataharikishavyo kiota chake, na kupapatika juu ya makinda yake, alikunjua mbawa zake, akawatwaa, akawachukua juu ya mbawa zake:*

<sup>40</sup> Huko sio kusoma sana Maandiko, bali ni Neno la Bwana. Limetosha hapo hata, labda, Mungu atatupatia muktadha kutoka kwenye hili, katika dakika ishirini ama thelathini zijazo, ambao utawafanya watu kuamka na kumwazia Bwana Yesu.

<sup>41</sup> Mnajua, siku moja, nilisoma hadithi, miaka michache iliyopita, katika *Maisha Ya Abraham Lincoln*. Kulikuwako na mtu gerezani, naye alikuwa chini ya shtaka la shirikisho, naye alikuwa apigwe risasi. Basi rafiki yake mwema akamwendea Rais, Abraham Lincoln, Mkristo mzuri sana. Naye akasema,

“Bw. Lincoln, ninajua ya kwamba wewe ni mtu mwema, kwamba wewe ni Mkristo. Na chini ya shtaka hili la shirikisho, mtu huyu amevunja sheria ya kanuni za jeshi. Yeye ni rafiki yangu. Hakumaanisha kufanya hivyo. Ana hatia ya kufanya hivyo. Hakumaanisha kufanya hivyo. Naomba tafadhali... Wewe ndiye mtu pekee ambaye anaweza kuyaokoa maisha yake. Waweza kuyaokoa maisha yake tafadhali?” Kwa fadhila ya Bw. Lincoln akachukua kalamu yake ya unyoya na kuandika kwenye kipande cha karatasi, kwa sababu hakuwa kwenye dawati lake wakati huo, kutia muhuri rasmi. Na kwa hivyo akaandika juu yake, “Namsamehe mtu huyu,” na kutia saini jina lake, “Abraham Lincoln.”

<sup>42</sup> Huyu rafiki wa thamani wa mtu huyu akatimua mbio kadiri alivyoweza, akaenda gerezeni, na kusema, “Loo, rafiki yangu, uko huru. Uko huru. Hili hapa jina la Rais kwenye kipande hiki cha karatasi. Umesamehewa.”

<sup>43</sup> Basi yule mtu akasema, “Usinidhihaki, kwa kuwa niko tayari sasa kufa, kwa sababu nimehukumiwa kifo. Nawe huyu hapa unakuja kunidhihaki na kipande cha karatasi. Kama kipande hicho cha karatasi kilikuwa ni msamaha wa Abraham Lincoln, kingepambwa kote kwa mihuri na kadhalika.”

<sup>44</sup> Akasema, “Bwana, hili ni jina la Rais. Umesamehewa.” Naye yule mtu akaupa kisogo wala hangeusikiliza.

<sup>45</sup> Kesho yake asubuhi, kwenye mapambazuko, huyo mtu alipigwa risasi mbele ya kikosi cha wapiga risasi. Sasa, huu hapa msamaha kutoka kwa Rais, ambao unasema, “Msimuue huyo mtu,” uliosainiwa siku moja. Kesho yake, mtu huyo akapigwa risasi.

<sup>46</sup> Basi kesi hiyo ilisikizwa katika mahakama ya shirikisho. Ndipo wakati mahakama, Mahakama ya Shirikisho la Marekani iliposikiliza kesi hiyo, basi huu hapa uamuzi wa hiyo mahakama. “Msamaha sio msamaha isipokuwa upokelewe kama msamaha.”

<sup>47</sup> Basi hivyo ndivyo Neno la Mungu lilivyo. Ni uponyaji kwako, ukilipokea kama uponyaji. Ni msamaha kwako, ukilipokea kama msamaha. Kila baraka *Hapa* ndani ni yako kama ukiipokea jinsi ambavyo Mungu ameandika.

*Mfano wa tai ataharikishavyo...kiota chake, na kupapatika juu ya makinda yake,...anawatwaa juu ya mbawa zake, na anawachukua.*

<sup>48</sup> Ni mara ngapi nimewazia jinsi Mungu alifananisha urithi Wake, na tai! Nami naona, katika Biblia, kwamba Mungu anajiita Mwenyewe tai. Yeye ni Yehova tai. Basi angefanyaje hivyo?

<sup>49</sup> Kwa hiyo, mimi ni mwanamaumbile. Kwa hiyo mimi... Biblia yangu ya kwanza ilikuwa ni maumbile. Kama utaangalia tu jinsi maumbile yanavyofanya kazi, unaweza kumwona

Mungu. Popote utazamapo, utamwona Mungu, kama ukiwa na Mungu moyoni na kuangalia. Sasa, wanapozungumza juu ya roho ya marehemu kuzaliwa tena katika mwili mwingine na kadhalika, huo ni ujinga; haiwezekani.

<sup>50</sup> Tunaona kwamba mmea hufa, unaingia ardhini; mbegu inaoza, inaishi tena. Ni ufufuo. Nao Ukristo wote umewekwa msingi juu ya ufufuo. Nasi tunaweza kuona ya kwamba hiyo ni kweli; kifo, kuzikwa, ufufuo; viangazi, baridi kali. Maumbile yote yanapatana moja kwa moja.

<sup>51</sup> Biblia yangu ya kwanza, ilikuwa ni kuangalia jinsi miti hiyo inavyokufa, jinsi chipukizi zinavyochipuka tena; jinsi ambavyo upepo ungevuma juu yake, ungerudi tena; jinsi maskini lile ua lilivyokufa, likaishi tena. Na vitu hivyo vyote mbalimbali, ilinifanya nijue kwamba kulikuwa na nguvu za ufufuo mahali fulani.

<sup>52</sup> Sasa, mti una maisha yanayoendelea. Sisi tuna Uzima usiopatikana na mauti. Mti utafikia mwisho wake. Kamwe hatuwezi; tunao Uzima usiopatikana na mauti.

<sup>53</sup> Sasa, nilianza kuwachunguza tai wakati niliposoma hili. Vipi kuhusu tai? Ninaona kwamba tai ni ndege wa kipekee sana. Anaweza kuruka juu kuliko ndege mwingine yeyote aliyepo. Yeye ni ndege aliyeumbwa maalum. Hujenga kiota chake katika miamba, huko juu kabisa. Yeye ni ndege wa kipekee sana. Na jambo lingine, manyoya yake yameshika sana huwezi, ni vigumu, huwezi kuyang'oa kwa koleo. Yeye ni ndege mkubwa mno, mmoja wa walio wakubwa kuliko wote waliopo. Naye ni ndege wa kipekee sana. Lakini ameumbwa maalum kwa sababu ana kazi maalum ya kufanya.

<sup>54</sup> Neno *tai* linamaanisha “rarua kwa mdomo.” Naye hula kwa mdomo. Jambo zuri sana la Neno la Mungu, hula kutoka kinywa hadi kinywa, Mungu akiwalisha watoto wake.

<sup>55</sup> Halafu yeye hujenga kiota chake juu, naye analo hilo kwa kusudi fulani, na kadhalika. Sasa, kama...Tai alikuwa na mbawa kubwa zenye nguvu. Hiyo ni kwa ajili ya ukombozi.

<sup>56</sup> Na jambo lingine analofanya tai, ambalo ni la kigeni, yeye huufanya upya ujana wake. Tai, baada ya muda mrefu sana, huzunguka tu na kurudi akawa tai mchanga tena, hujirudisha moja kwa moja. Anaufanya upya ujana wake.

<sup>57</sup> Huo ni mfano mwingine wa Kanisa, wa watu wa Mungu. Tutashuka chini kabisa na kidogo tunachacha, halafu, mara, Roho Mtakatifu anakuja na kutufanya upya tena. Mungu, akifanya upya ujuzi na vijana wa Kanisa Lake, akiwapa ujuzi mpya. Huo ni mfano wa tai.

<sup>58</sup> Miaka kadha iliyopita, nilikuwa nikipanda farasi sana, ranchi, nasi tulikuwa juu ya Mto Troublesome huko Colorado. Shirika la Hereford hulisha kwenye malisho hayo ya Arapaho



kule, na kadhalika, na huko juu kuizunguka hiyo milima. Nasi tulikuwa tukiwapeleka ng'ombe huko juu. Ndipo basi, mwakani, ingetulazimu kuwatafuta tena, tuwapeleke katika Msitu wa Taifa. Kisha tungekuza nyasi zetu kavu huko chini kabisa, tupate kuwalisha, kwenye msimu wa baridi kali.

<sup>59</sup> Na ningeenda huko nje kila mwaka, kuwinda. Ningali nawinda, bado. Ndipo rafiki yangu, tungerudi, baada ya watu wote kutoka mijini kufika kule na kurusharusha risasi, wanyama wa kike, na watoto wao, na ng'ombe wachanga, na dume wakongwe wa kulungu wanaojikokota huko chini. Mbona, sikuzote sisi tunaenda huko nyuma kabisa, juu, ambako huwezi kuingia, na kupiga kambi huko nyuma. Anachukua upande wa mashariki, mkondo wa mashariki au magharibi, mojawapo, nami nitachukua huo mwingine. Itachukua siku kadhaa kabla hatujakutana.

<sup>60</sup> Wala sitasahau kamwe, mwaka mmoja, theluji haikuwa imeanguka, ilikuwa mnamo Oktoba wakati huo msimu ulipoingia.

<sup>61</sup> Na iwapo theluji itaanguka huko milimani . . . Mbona, labda, mnamo Oktoba, kutatokea a—alasiri nzuri kweli kweli, labda katika saa nyingine moja theluji itakuwa ikianguka. Kisha itainyeshea, halafu jua litachomoza, badiliko tu la hali ya hewa. Lakini basi, theluji inapokuja, inawafukuza kulungu na paa, hao wakubwa ambao wanaishi kule juu, mbali na kelele za ustaarabu, inawafukuza wakaingia mabondeni. Huko ndiko kwa kawaida unapata nyara.

<sup>62</sup> Mwaka huu, theluji haikuwa imekuja bado, nami nilikuwa huko juu. Nami nilikuwa nimemwacha farasi wangu maili kadhaa huko nyuma, na kumfunga, apate kuwa na nafasi tele; nyasi kavu, aweze kula. Nami nilikuwa nimeenda kote nikazunguka mpakani mwa msitu, huko juu, nikiangalia.

<sup>63</sup> Alasiri hiyo ikatokea dhoruba ikienea milimani, na—na ngurumo ya radi, na radi ikimulika. Nami nilikuwa nimefika nyuma ya mti mmoja. Basi nikasimama nyuma ya huo mti mpaka dhoruba ilipokwisha, nikashuka msituni. Kulikuwa na uwazi huko chini. Nami nilikuwa nimesimama nyuma ya mti, nikingojea mpaka dhoruba ipite; nikisimama pale, nikiwazia. Nami nilikuwa nimeiegemeza bunduki yangu kwenye m—mti. Ndipo basi dho—dhoruba ilipokwisha . . . Nilikuwa nikiwazia juu ya Mungu, jinsi alivyokuwa ni wa ajabu.

<sup>64</sup> Basi dhoruba ilipokuwa ikiendelea, upepo baridi uliingia, nao ukagandisha wingi wa maji kwenye miti isiyokauka, kama michirizi ya theluji iliyoning'inia. Ndipo jua lilipochomoza, huko nyuma kabisa, magharibi, ningeweza kuona jua likichungulia tu kupitia kwenye nyufa za mlima, na kuonekana kama jicho la Mungu.

<sup>65</sup> Mnajua, Mungu yuko kila mahali. Unaweza tu kumwona, mahali popote, iwapo tu utamtafuta. Yeye yuko. Huna budi kumwona. Atakuwa hapa. Yuko hapa sasa hivi. Kama tu utaangalia pande zote, utamwona.

<sup>66</sup> Ndipo basi nilipokuwa nimesimama pale, niliangalia hayo—hayo machweo ya jua. Basi nikainua mikono yangu, na kusema, “Ee Yehova Mungu mkuu, macho yako yanaangalia huku na huko, kote duniani.”

<sup>67</sup> Mara nikasikia kilio kutoka kwa kulungu du—dume. Alitenganishwa na kundi lake, katika hiyo dhoruba, naye alikuwa akitoa huo mlio mkali sana wa sauti namna hiyo. Nikasikia hilo kundi likimjibu, hapa mahali pengine. Na huko juu ubavuni mwa mlima, maskini mbwa mwitu wa kijivu akaanza kulia; mwenziwe akamjibu, huko chini kabisa. Nikaangalia pande zote, bondeni, kutoka kwenye mlima mmoja, ng’ambo ya hilo bonde, palikuwako na upinde wa mvua. Vema, kila mahali tu nilipoangalia, palikuwapo na Mungu.

<sup>68</sup> Mama yangu ni nusu Mhindi. Alitoka kwenye risavu, na ni Mhindi wa Cherokee. Naye mama yake alipata malipo ya uzeeni. Uongofu wangu kamwe haukuondoa hilo kwangu. Kuna kitu kuhusu misitu na nyika nipendacho.

<sup>69</sup> Nilipomsikia maskini mbwa mwitu huyo akilia, na mwenziwe akijibu, machozi yalianza kutiririka mashavuni mwangu. Nikamsikia huyo kulungu dume akilia kule juu, kwa ajili ya kundi lake. Likajibu. Nikaangalia upinde wa mvua. Nikasema, “Naam. Yule pale Mungu tena.” Yeye ni Alfa na Omega. Yeye ni rangi, lile agano, katika upinde wa mvua. Mungu yuko kila mahali, kama tu ukimtafuta pande zote.

<sup>70</sup> Nilifurahi sana! Nikainua tu mikono yangu, huku machozi yakitiririka mashavuni mwangu. Nikakimbia-kimbia, kuzunguka na kuzunguka mti huo. Nilikuwa tu na wakati mzuri sana, wala hakuna mtu maili thelathini kutoka kwangu; nikiruka-ruka tu juu chini, na kupiga mayowe kwa sauti yangu yote. Kwa kweli, kama kungekuwa na mtu akiniangalia, wangaliwazia mtu fulani kutoka kwenye hospitali ya wendawazimu alikuwa huko nje. Ila sikuwa nikijali. Nilikuwa na wakati mzuri. Nilikuwa nikimwabudu Bwana, Mungu wangu. Haikuleta tofauti yoyote kwangu kile mtu mwingine yeyote alichowazia. Nami nilikuwa tu na wakati mzuri, kuzunguka tu mti ule, tena na tena na tena. Ningesimama, nimsikilize yule mbwa mwitu, na kusikiliza hicho. Kisha nipige mayowe tena, nizunguke mti huo, tena na tena.

<sup>71</sup> Ndipo ni—nikakisisimua kitu fulani. Na huyo hapo maskini kuchakulo wa misonobari. Sijui kama mnajua hao ni nini hapa Oklahoma, au hamjui. Maskini kitu kidogo tu cha makelele yapata urefu *huo*. Yeye ndiye polisi mwenye koti la samawati wa mwituni. Yeye ananinii tu... Anapiga kelele nyingi sana,

na hakuna chochote kwake. Ndipo akaruka juu ya kisiki, na akaanza kupayuka, akapayuka, akapayuka, kwa nguvu tu kadiri alivyoweza. Nami nikawazia, “Huna haja ya kusionywa. Ninamwabudu Bwana. Kwani hupendi hilo? Hebu angalia hili.” Nikazunguka, na kuzunguka, na kuzunguka, na kuzunguka tena, nikaenda, mbio kadiri nilivyoweza. Nami nikasema, “Si ni ajabu hiyo? Muumba wako; Mungu wangu!” Sisi hapa tunaenda tena, kuzunguka, na kuzunguka, na kuzunguka namna hiyo.

<sup>72</sup> Ndipo nikamwona yule jamaa mdogo akiweka kichwa chake kidogo upande mmoja, na kuangalia chini katika uwazi huo. Haikuonekana kana kwamba nilikuwa nimemsisimua. Kuna kitu kingine kilichomsisimua. Vema, nikawazia, “Sidhani ninatenda kigeni. Kwa sababu, sitendi kigeni, kwangu mimi. Nami najua Yeye ananibariki, kwa hivyo hata afadhali ujiunge nami moja kwa moja.”

<sup>73</sup> Basi ilitokea kwamba niliangalia. Kumbe dhoruba ilikuwa imemlazimisha tai mkubwa kushuka chini. Nayo ilimlazimisha kushuka ndani. Alikuwa ameshuka chini, labda akila. Hakuweza kujiendeleza, juu yake, kupanda juu ya dhoruba, kwa hivyo ikamlazimu kushuka chini vichakani. Naye huyo hapo, chini ya hivi—hivi vichaka hapo.

<sup>74</sup> Kumbe huyo ndiye aliyekuwa akimsisimua maskini huyo kuchakulo. Naye alikuwa akimwangalia kwa makini sana, namna hiyo, akipayuka, payuka, payuka, kupiga gumzo, kama kwamba atamraria yule tai vipande vipande. Vema, hakuwa mkubwa wa kutosha kuraria chochote vipande vipande. Kwa hivyo alikuwa amesimama juu ya kile kisiki, mkia wake mdogo umejikunja namna *hiyo*, kupayuka, payuka, payuka tu; kupayuka, payuka, payuka. Nikawazia, “Vema, usisimkwe. Hata kudhuru.”

<sup>75</sup> Ndipo tai huyo mkubwa akaruka juu ya tawi, namna *hiyo*. Nami nikawazia, “Ee Mungu, Wewe yule kule, katika wito huo wa mbwa mwitu. Wewe huyo hapo, hapa, katika wito wa porini. Wewe yule kule, katika machweo ya jua. Wewe yule kule, katika upinde wa mvua. Kwa nini ukamweka yule tai mbele yangu? Yule, yule tai anafanya nini pale? Siwezi kukuona katika yule tai.”

<sup>76</sup> Nikamwangalia huyo tai. Nikasema... Nikamwangalia, macho yake makubwa ya kijivu. Hakuwa akimjali huyo kuchakulo wa misonobari, sana. Alikuwa akiniangalia. Ningeweza kuona macho hayo makubwa mno yakinitazama. Nami nikawazia, “Vema, naam, ninaweza kumwona Mungu katika tai huyo, kwa sababu yeye haogopi. Kuna kitu fulani kumhusu, kwamba haogopi.” Nikasema, “Nitajaribu, nione kama anaogopa.”

<sup>77</sup> Nikasema, “Aisee, jamani, unajua ningeweza kukupiga risasi?” Nikasema, “Hii ni bunduki yangu. Ningeweza kukupiga risasi.”

<sup>78</sup> Akaniangalia tu, namna *hiyo*. Nikaendelea kumwona akiyahisi mabawa yake. Nikasema, “Kumbe. Hiyo ndiyo sababu. Huogopi, kwa sababu Mungu alikupa mabawa mawili. Nawe unajua, vizuri kabisa, ungeweza kuwa kule msituni kabla hata sijaweza kuishika bunduki hiyo mkononi mwangu.” Nikawazia, “Kama ungeweza kutumainia mabawa yako uliyopewa na Mungu, kutoka katika hatari, ni zaidi sana vipi Kanisa, likiwa na Roho aliyetolewa na Mungu, Roho Mtakatifu miongoni mwetu, kuondokea mambo, kutoka ndani yake, namna hiyo.” Nikamwangalia, jinsi alivyoyahisi hayo mabawa. Maadamu . . .

<sup>79</sup> Mtu mmoja aliniambia wakati mmoja, “Ndugu Branham, huogopi kuwa utakosea?” La, bwana, siogopi maadamu ninaweza kuhisi kitu Fulani hicho karibu nami. Hiyo ni kweli. Hiyo ni sawa. Maadamu Yeye yuko hapo, ni Yeye anayelifanya.

<sup>80</sup> Nami nikamwangalia huyo tai kwa muda mrefu. Naye akaona ya kwamba nilimpenda kupita kiasi, singemdhuru. Na kwa hiyo hakuniogopa, bali alipata kichefuchefu kwa huo mpayuko, mpayuko, mpayuko; mpayuko, mpayuko, mpayuko. Basi akachoshwa nao, kwa hivyo akafanya tu mruko mmoja mkubwa mno, akapigapiga mbawa zake karibu mara mbili. Na ndipo nikaona ni kwa nini alinikatisha nikipiga makelele. Tai huyo mkubwa hakupigapiga mbawa zake tena. Alionekana tu kujua jinsi ya kuweka mbawa zake. Na kila wakati upepo ungeingia, angepanda juu zaidi. Kisha upepo ungeingia, angepanda juu zaidi. Nami nikasimama pale na kumwangalia mpaka akawa chembe ndogo tu. Nikasema, “Ee Mungu, jambo ndilo hilo.” Alichoshwa na huo mpayuko, mpayuko, mpayuko.

<sup>81</sup> Sio, “Kimbia kutoka kanisa hadi kanisa. Jiunge na *hili* na ujiunge na *lile*.” Ni kujua tu jinsi ya kuweka mabawa yako katika nguvu za Roho Wake Mtakatifu. Anapokuja amepanda, nawe panda tu, panda, panda tena na tena na tena. Ondoka kwenye huku kupayuka, payuka, “Siku za miujiza zimepita. Hakuna kitu kama Roho Mtakatifu. Nyote mmekosea, katika *Hili*. Hakuna kitu kama uponyaji wa Kiungu.” Endelea tu kupanda, juu yake. Acha tu Roho Mtakatifu apande ndani, na apande aende Zake. Endelea tu, huko juu kabisa na juu zaidi, mpaka ufikie umbali usioweza kusikia. Jamani!

<sup>82</sup> Mungu alimwumba tai. Sasa, ikiwa hakuwa na . . . Kama mwewe alijaribu kumfuata tai, angetenguka hewani. Kunguru akijaribu kumfuata, manyoya yake yangepukutika. Yeye ni ndege aliyeumbwa maalum.

<sup>83</sup> Mungu aliwafananisha tai Wake na manabii Wake. Nabii hupanda juu akaingia kwenye maeneo ambamo anaweza kuangalia mbali mno.

<sup>84</sup> Sasa, kama tai ana mabawa makubwa, yenye nguvu ambayo yanaweza kumpandisha huko juu. Pia, macho yake yasipolinganishwa na mbawa zake, angekuwa kipofu afikapo huko juu. Hiyo ndiyo sababu mwewe, akijaribu kuwa tai, alipofika juu sana, hangeweza kuona, kwa vyovyote vile, kwa hivyo isingemfaa kitu kupanda juu. Mnaona? Yeye ni ndege aliyeumbwa maalum.

<sup>85</sup> Naye Mkristo ni mtu aliyeumbwa maalum. Hiyo ni kweli kabisa. Hakuna haja ya kwenda kanisani, isipokuwa umepata Kitu ambacho kinakwambia kuwa yote yapo. Unaona? Ni jambo maalum ambalo Mungu anakufanyia.

<sup>86</sup> Tai huyo anaweza kwenda juu sana hata usiweze kumwona, naye anaweza kuona kitu chochote kinachotembea ardhini, kitu kilicho kidogo sana; jicho lake ni kubwa mno.

<sup>87</sup> Siku moja, miaka mitatu au minne iliyopita, mimi na msichana wangu mdogo tulikuwa tukitembea kwenye bustani ya wanyama huko Cincinnati. Nilikuwa nao kule Jumamosi moja alasiri, nikiwaonyesha vitu mbalimbali. Nami na mtoto Sarah tukatembea huko, alikuwa msichana mdogo sana wakati huo, yapata tu umri wa miaka mitatu. Nasi tulikuwa tukitembea huko. Na kulikuwa na tai mkubwa kwenye kizimba.

<sup>88</sup> Nami sikuzote nilichukia kuona wanyama wamefungiwa kizimbani. Sijui, nachukia tu kumwona kurumbizi... Sasa, siwatupilii mbali, kasuku wenu na kadhalika, bali sipendi kuona chochote katika kizimba. Najua jinsi ilivyo kufungwa kwenye dini ambapo huna uhuru wowote. Sasa, mimi—mimi—mimi nataka... Napenda kuwa huru.

<sup>89</sup> Halafu, ni kama tu kuwapa kurumbizi wako vitamini zote uwezazo, kufanya manyoya mazuri na mabawa mazuri, na kisha kumweka kizimbani. Inamfaa nini?

<sup>90</sup> Kuna faida gani kuwapeleka wahubiri kwenye seminari na kadhalika, na kuwaelimisha, kila kitu namna hiyo, na kisha uwafungie, kwa kusema, “Siku za miujiza zimepita. Hakuna kitu kama hicho”? Kuna faida gani kuwaelimisha? Ninii...

<sup>91</sup> Ndugu, napenda kitu huru, ambapo unaweza kuruka na kujifanyia mazoezi, dini ambayo inakuacha uwe huru.

<sup>92</sup> Nilimwona tai huyu mkubwa. Walikuwa ndio kwanza wamemkamata, wakamweka kwenye kizimba. Nilifikiri hiyo ilikuwa ndiyo tamasha ya kuhuzunisha sana niliyopata kuona. Jamaa huyo mkubwa mno, alikuwa amelala pale sakafuni, nilipokaribia, mbawa zake kubwa mno zimekunjuliwa. Manyoya yalikuwa yameng’olewa kichwani mwake, na shingoni mwake na juu ya ncha za mbawa zake. Nikamwangalia.

<sup>93</sup> Akatambaa kizimbani. Akaangalia nyuma kizimbani, namna *hiyo*. Huyu hapa anakuja, naye akakigonga kizimba hicho kwa kichwa chake na mbawa zake, akipigapiga tu.

Manyoya yangeruka. Angerudi aanguke. Angeinuka tena. Akarudi *hivi*. Angeangalia juu. Naye angeruka mbio kadiri alivyoweza, na kuzigongesha mbawa zake na kichwa chake humo, akaanguka tena. Akalala pale, na macho yake makubwa yakizunguka-zunguka, akiangalia juu.

<sup>94</sup> “Loo,” nikawazia, “hiyo ni moja ya tamasha za kuhuzunisha sana mtu angaliweza kutazama.” Yeye ni ndege wa kimbinguni. Alizaliwa apate kupanda mbinguni. Na hapa, kwa ujanja na hila za mwanadamu, amefungiwa kizimbani. Hawezi. . . Yeye ni ndege wa kimbinguni. Hajui lolote kuhusu ardhi, hata. Inambidi kuishi mbinguni. Amelala pale, akiangalia juu ambako kweli anapaswa kuwa, ambako moyo wake unatamani kuwa, lakini kuna vizuizi kati yake na huko.

<sup>95</sup> Nilidhani hiyo ilikuwa tamasha ya kuhuzunisha, mpaka wakati mmoja nikawaona wanadamu, ambao Mungu aliwaumba katika mfano Wake, wamefungiwa kwenye madhehebu na kadhalika ambayo hayakuamini katika uponyaji wa Kiungu, wamefungiwa katika maeneo ambayo hawangeweza kuwa huru. Wamezaliwa kutoka Mbinguni. Roho aliyetumwa na Mungu yuko ndani yao, namna hiyo, lakini yanawafungia kabisa wasiweze kutoka. Kuona wanaume na wanawake wakitembea mitaani, wamevaa kizinifu, katika vilabu, wamefungiwa kabisa. Ambapo, wanapaswa kuwa huru, wana na binti za Mungu. Na kuzigongesha bongo zao kabisa, karibu hivyo, kwenye kitu fulani, wakijaribu kuwa huru.

<sup>96</sup> Ee Mungu, kama ningalikuwa na nguvu, ningeninii. . . ama mamlaka, ningemnunua maskini tai huyo na kumwachilia aende, nimwache aende zake huru atakako. Hilo ni jambo la kuchukiza, kumfungia kizimbani.

<sup>97</sup> Lakini ni baya jinsi gani, kuwachukua wana wa Mungu na kuwafungia mahali ambapo wananinii. . . Kweli, roho yao inataka kutoka nje na kufanya kitu fulani. Kisha mtu fulani anasema, “Hakuna kitu kama uponyaji wa Kiungu. Hakuna kitu kama nguvu za Roho Mtakatifu. Hakuna kitu kama *Hiki*.” Wanawaweka kwenye kizimba. Ndugu, hebu nikwambie, kuna uhuru.

<sup>98</sup> Wakati mmoja mtu alimnasa maskini kunguru mmoja na kumfunga, maana alikuwa kwenye shamba la mahindi. Naye. . . Ndipo ndege wakaanza kuruka juu yake, na kusema, “Hima, Kunguru Johnny, twende Kusini. Twende Kusini. Majira ya baridi kali yanakuja.”

<sup>99</sup> Alidhoofika sana, alitembea kwa shida. Yupo mtu mzuri aliyepitia pale, siku moja, na kusema, “Maskini kunguru huyo!” Naye akamfungulia tu.

<sup>100</sup> Basi alipomfungulia, wale kunguru wengine wakaja huko, wakasema, “Hima, Kunguru Johnny, twende Kusini.”

<sup>101</sup> Lakini yeye—yeye alikuwa amefungwa kwa muda mrefu sana, mpaka, alizunguka hapo tu, kasema, “Siwezi kwenda. Siwezi kwenda.” Hakujuua alikuwa huru.

<sup>102</sup> Hivyo ndivyo mwanadamu alivyo siku hizi. Hujui kwamba Yesu Kristo alikuweka huru, ndugu. Hebu tutoke humo. Hebu tufike mahali fulani. Mungu alituweka huru. Msife kwa njaa. Mungu anazo baraka za kipentekoste kote angani, na—na rasilimali zisizotumiwa bado za wema Wake. Hebu tuziendee. “Yeyote atakaye, na aje. Na aje, anywe kutoka kwenye Maji ya Uzima, bure.”

<sup>103</sup> Tai, hujenga kiota chake juu katika mwamba. Yeye ni kama—yeye ni kama Kanisa. Kanisa la Yesu Kristo ni Kanisa lililowekwa juu ya kilima, linalotoa Nuru. Liko juu. Lina shauku kuu. Linapaswa kuwa na ukaguzi wa hali ya juu, matarajio, hasa. Linapaswa kuwa na matarajio makuu, kwa sababu tumekuwa tukimtarajia Mungu kufanya jambo fulani.

<sup>104</sup> Kama ukija hapa alasiri ya leo, ukisema, “Vema, nitapanda kule. Kama nikiingia kwenye mstari wa maombi, sawa. Vema, endapo ataniambia kuwa mimi ni mzima, iwapo Bwana atanijulisha.” Loo, usiwe na matarajio kama hayo. “Lakini asipofanya hivyo, basi sitapata kitu.” Matarajio yako sio mengi.

<sup>105</sup> Njoo kanisani, alasiri hii, ikiwa wewe ni mgonjwa, useme, “Ninatarajia kwenda nyumbani mzima. Sitaondoka mpaka litakapotendeka.” Ikiwa huna Roho Mtakatifu, sema, “Nitabaki hapa na kuozea mahali hapa, ama nitampata Roho Mtakatifu. Nimekuja hapa miongoni mwa watu wa Roho Mtakatifu. Nimekuja hapa alipo Roho. Nitabaki hapa hapa mpaka nimpate.”

<sup>106</sup> Kuwa kama mzee Buddy Robinson alivyokuwa, aliposhuka kwenye lile shamba la mahindi. Akasema, “Bwana, usiponipa Roho Mtakatifu, utakaporudi duniani utapata lundo la mifupa ya Buddy Robinson limekaa hapa.” Hiyo ndiyo njia ya kulifanya. Hiyo ni kweli kabisa.

Tunalichukulia hivi hivi sana.

<sup>107</sup> Mtu mmoja, wakati mmoja, alikuwa akijaribu kumtafuta Mungu. Na kila wakati angesema, “Nimeokoka,” ibilisi angesema, “Hapana, hujaokoka.” Siku moja akapigilia kigingi chini. Akasema, “Shetani, tangu sasa na kuendelea, nitaelekeza kwenye kigingi hiki. Hapa ndipo nilipotimiza matakwa ya Mungu, papa hapa.”

<sup>108</sup> Wewe pigilia kigingi chako chini, papo hapo karibu na kiti chako, alasiri ya leo, ukisema, “Shetani, papa hapa ndipo kila shaka litakapobakia. Nami nitaruka pamoja Naye, alasiri ya leo. Nitakubali kile hasa alichoniambia ningeweza kufanya.” Ikiwa utaamini.

<sup>109</sup> Maskini tai huyu, anapojiandaa kujenga kiota chake, yeye huenda juu sana kwenye miamba. Naye anajenga kiota chake huko juu. Kwa sababu ananinii... Anataka kuyalinda makinda wake.

<sup>110</sup> Hivyo ndivyo Mungu afanyavyo. Yeye huliinua Kanisa Lake kufikia mahali fulani, ikiwa tu utamruhusu, basi atakuweka mahali ambapo utakuwa mbali na koho wa duniani. Hakika, atakuweka.

<sup>111</sup> Ni tofauti jinsi gani na kuku! Kuku ni ndege, pia, lakini hujenga kiota chake nje kwenye kitalu mahali fulani, chini ardhini ambako cheche na nyoka, na chochote kile, kinaweza kuwapata makinda wake. Hajui lolote kuhusu ya kimbinguni. Hata hivyo, yeye ni ndege; labda, ndugu wa kimadhehebu, bali yeye ni—bali yeye ni—yeye yuko ardhini. Hajui lolote kuhusu ya kimbinguni, kuruka juu, mahali fulani huko juu sana ambapo ni samawati na panapendeza.

<sup>112</sup> Maskini mama tai, wakati anapotengeneza kiota chake. Jinsi nimewaangalia mara nyingi, wakitoka kwenda kuokota vijiti vikubwa, na kuvichomeka ndani ya hiyo miamba. Na kukivuta hapa na mdomo wao mkubwa, na kukifunga vizuri, na kuchukua matawi ya miiba na kukizungushia. Na ndani ya kiota kumetengenezwa na miiba, hasa, kuzifunga nguzo zilizo kubwa, pamoja, anazobeba kule juu. Lakini yeye hukikaza kiota hicho hata hakuna dhoruba inayoweza kukipeperusha.

<sup>113</sup> Nina furaha, “Juu ya mwamba huu nitalijenga Kanisa Langu, na malango ya kuzimu hayawezi kulishinda.” Mwamba wa aina gani? Ufunuo wa kiroho.

“Watu hunena Mimi Mwana wa Adamu kuwa ni nani?”

“Wengine wanasema ‘Eliya,’ wengine wanasema ‘Musa.’”

“Lakini nyinyi je?”

Petro alisema, “Wewe ndiye Kristo, Mwana wa Mungu.”

<sup>114</sup> “Heri wewe, Simoni, mwana wa Yona. Mwili na damu havikukufunulia hili. Kamwe hukujifunza hili katika seminari. Hukujifunza hili kwa mtu kukwambia, ila Baba Yangu aliye Mbinguni amekufunulia hili. Juu ya mwamba huu nitalijenga Kanisa Langu, na malango ya kuzimu hayawezi kulishinda. Dhoruba za maisha hazitalitikisa kamwe.” Hiyo ndiyo sababu Yeye alisema alikuwa Tai. Alijenga kiota.

<sup>115</sup> Ndipo maskini mama tai, akijiandaa kwa watoto wake kuzaliwa, yeye huondoka na kuokota kila kitu awezacho, majani mororo. Anachukua mdomo wake mkubwa na kuviweka tena pembeni, na kuweka miiba yote, kote, isije ikawachoma watoto wake. Anatoka na kumwinda mwana-kondoo, ama labda sungura, ama kitu fulani, anakula nyama yake; kisha anaichukua hiyo su—sufu, anatoa sufu yake, na kukitonea hicho



kiota. Loo, anakifanya kizuri kweli, kwa ajili ya watoto wake wanaokuja.

<sup>116</sup> Hivyo ndivyo Yehova Tai afanyavyo, pia. Yeye hukitengeneza vizuri sana. Loo, jamani! Wakati mtoto mpya anapozaliwa, mbona, katika Ufalme wa Mungu, yeye huninii tu. . . Anafikiri anaweza kutembea, lakini sikuzote anajigongagonga huku na huku, na kukimbia kote. Lakini ana wakati mzuri. Yuko kwenye kiota, ambamo kote kumetandazwa manyoya, mwajua. Ile—ile mianguko haimdhuru. Na kwa hiyo hivyo ndivyo mama Yehova Tai afanyavyo. Anakitengeneza kiota chake vizuri na kukijaza sufu, kwa ajili ya watoto Wake watakozaliwa.

<sup>117</sup> Baada ya kitambo kidogo, mayai yanakuja, kisha anakuja mwana tai. Ndipo anashuka, yeye na baba tai, nao wanawalisha watoto wao wote, mpaka wanakuwa wakubwa vizuri. Ndipo wanapofikia ukubwa fulani. . .

<sup>118</sup> Sasa, mama tai atakuwa na hakika kwamba hao tai hawatakuwa vyovyote kama kuku. Hiyo ni kweli. Yeye hawataki wafungwe duniani. Wao ni tai, naye anajua wao ni tai.

<sup>119</sup> Hivyo ndivyo Yehova Tai afanyavyo. Hataki sisi tuwe kuku, kuku wa kitalu. Anataka tuwe tai, huko juu katika bluu, asili yetu iwe huko juu ambako tuko huru. “Yeye ambaye Mwana amemweka huru ni huru kweli kweli.” Huko, anawataka huko juu. Kwa hivyo, siku chache. . .

<sup>120</sup> Jinsi nimewaangalia, mara nyingi sana! Siku chache kabla ya wakati wa kutaharikisha kiota kufika, yule maskini mama tai angepanda pale kando ya kiota hicho. Nimelala, siku nyingi, kwenye jua lenye joto, nikawaangalia, na kulia tu kama mtoto mchanga. Unaona, huyo mama tai mkubwa, hao ni wakubwa. Mama tai ni mkubwa kuliko baba tai. Baadhi ya mbawa zao zinakunjuka futi kumi na nne, ncha hadi ncha.

<sup>121</sup> Naye atapanda kule juu. Ataenda kwa mkogo, juu ya kiota hicho, namna *hiyo*. Naye atawaendea hawa watoto. Atatandaza mbawa zake kubwa na kupaza sauti. Ndipo anapofanya hivyo, wakati mwingine tai wadogo wataanguka kichalichali. Anawataka waanguke. Hivyo ndivyo anavyowataka wafanye. Kisha wataamka. Naye atapaza sauti. Kwa nini? Anawafundisha waijue sauti yake.

“Kondoo wangu wanaijua sauti Yangu.”

<sup>122</sup> Anawataka wajue ni kitu gani hapo wakati wa kupaza sauti utakapofika. Naye anapaza sauti. Loo, jamani! “Nataka mshike kila mlio wa sauti yangu,” anasema, “kwa sababu kuna ndege wala mizoga wengi sana. Nataka mjue ninyi ni tai. Nataka mwijue sauti ya tai.” Amina. Haleluya! “Nataka mjue sauti ya tai ni nini.”

<sup>123</sup> Kisha anatandaza mbawa zake kubwa, anasema, “Angalieni hapa. Ninajiandaa kuwapa mruko wenu wa kwanza wa peke yenu. Lakini, kwanza, ninataka muone jinsi nilivyo mkubwa.”

<sup>124</sup> Loo, ni tamu jinsi gani! Labda, wakati mwingine, ugonjwa unatugonga mgongoni, labda kitu kingine, wakati tunapoweza kutazama juu na kuchukua mbawa mbili kubwa za Yehova, Agano la Kale na lile Jipya, na kusema, “Jinsi Wewe ulivyo mkuu! Jinsi Wewe ulivyo mkuu, Bwana!”

<sup>125</sup> Loo, yeye anapenda kuwaonyesha. “Angalia hapa jinsi nilivyo na nguvu.” Anapaza sauti, “Hii ndiyo sauti yangu.”

<sup>126</sup> Basi mhubiri angeweza kusema, basi, kwamba tai huyo hapazi sauti vivyo hivyo kila siku, kila wakati alipopiga makelele? Hakika. “Ni yeye yule jana, leo, na hata milele.”

<sup>127</sup> Agano la Kale lilisema, “Mimi ni Yehova. Niliifungua Bahari ya Shamu. Niliwatoa wana wa Kiebrania kutoka katika tanuru iliyowaka moto. Mimi Ndimi niliyemfufua Mwana wa Mungu.” Haleluya! “Mimi Ndimi niliyemtuma Roho Mtakatifu, kwenye Siku ya Pentekoste.” Ukiangalia kupitia mbawa Zake kuu, hivi hupendi kuona Hilo? Si linaufurahisha moyo wako?

<sup>128</sup> Hao tai wadogo wanasema, “Loo, Mama, hakika tunakutumaini. Wewe ni mwenye nguvu na ni mkubwa.”

<sup>129</sup> Hebu toka nje usiku mmoja ukaangalie mfumo wa jua. Hapa siku moja, nilipandishwa Mlima Palomar. Na hapo, kupitia kwa darubini, ungeweza kuona miaka milioni mia moja na ishirini ya kipindi cha nuru. Fanya hesabu, ni maili ngapi, ni ngapi. Nuru husafiri upesi kiasi gani? Miaka milioni mia moja na ishirini ya kipindi cha nuru, na kupita hapo kungali kulikuwa na miezi, na nyota, na ulimwengu nyingi. “Jinsi Wewe ulivyo mkuu! Jinsi Wewe ulivyo mkuu!” Tai wake wadogo wakaanza kuangalia pande zote. “Jinsi Wewe ulivyo mkuu!”

<sup>130</sup> Hili hapa ua. Lilikufa. Likaingia ardhini, bali hili hapa linachipuka tena. “Jinsi Wewe ulivyo mkuu!”

<sup>131</sup> Huyu hapa maskini mzee aliyeliwa na kansa ambaye ni kivuli, ndipo anafanyiwa maombi. Baadaye, unamwona, mtu mkubwa mno mwenye uso mwekundu. “Jinsi Wewe ulivyo mkuu! Jinsi Wewe ulivyo mkuu!”

<sup>132</sup> Umwone maskini mwanamke mkongwe huko mtaani, asiystahili kutazamwa na mbwa. Hebu nguvu za Mungu zimvutie wakati mmoja, atapaza sauti, “Jinsi Wewe ulivyo mkuu!” Ataweka kando kila mzigo na dhambi imzingayo kwa upesi. Muda si muda wajua, ni mtu anayeonekana mtakatifu. Yuko huko nje na kitini cha Injili chini ya mkono wake, akifanya jambo fulani.

<sup>133</sup> Hebu huyo mwuza pombe haramu, huko chini pembeni, mtu huyo wa kuchukiza, hebu wakati mmoja aangalie juu na kuona. “Jinsi Wewe ulivyo mkuu!” Mwangalie akiacha kuuza wiski

yake, akiacha kunywa pombe na kuvuta sigara, sigara na biri zake, akiacha kusema uongo wake, na kadhalika. Naye huko nje mtaani, ameshika Biblia mkononi mwake, akiushuhudia utukufu wa Mungu, “Jinsi Wewe ulivyo mkuu!”

<sup>134</sup> Hebu Mungu alitandaze Agano hilo Jipya na la Kale juu yako, wakati mmoja. Uangalie kupitia kurasa Zake na kuona jinsi lilivyo. Utasikia Sauti ikipiga makelele kutoka Mle, ikisema, “Yeye yule jana, leo, na hata milele. Niliyowafanyia hao, nitakufanyia wewe. Nami ni yeye yule. Mimi ni Yehova. Sibadiliki.” Ninajisikia kubarikiwa sana sasa hivi. Loo, jamani! Jinsi ninavyojua Hilo vema. Ni Ukweli.

<sup>135</sup> Sasa, mama ameyakinia, hao watoto wa tai hawatakuwa kuku. Lakini ameyakinia kwamba wasiwe. Mnajua vile afanyavyo basi? Baada ya kwenda kwa mikogo huku na huku kiotani, na kutandaza ninii zake... Kasema, “Angalia hapa, kipenzi, jinsi mimi nilivyo mkuu. Tazameni hapa. Mnapaswa kunitumaini. Nitawapeleka mahali ambapo itawabidi kunitumainia.”

<sup>136</sup> Ninajuaje kwamba Mungu hajawatuma wagonjwa humu ndani alasiri ya leo, vivyo hivyo? Akuweke mahali ambapo daktari... Unasema, “Mimi ni Mkristo, Ndugu Branham.” Ninajua hivyo. “Nami ninaye Roho Mtakatifu, nami huyu hapa, nikiteseka.”

<sup>137</sup> Unajuaje kama Yehova hajaribu tu kukufanya uangalie kupitia kwenye hizo mbawa uone jinsi Yeye alivyo mkuu? “Jinsi Mimi nilivyo mkuu! Nitakufanyia jambo fulani, hata itakubidi kunitumainia.” Haya basi. “Nami nataka ujue unachotumainia, kwanza. Unaona mbawa Zangu kubwa?”

<sup>138</sup> Halafu, baada ya siku chache, unajua mama huyo anafanya nini? Maadamu kitanda hicho kimekuwa chororo, maskini hao tai wadogo hawataki kukiacha. Kweli. Unajua afanyacho? Ndipo anaingia mle ndani kabisa, na kuchukua mdomo wake na kung’oa kila chembe ya sufu hiyo kutoka humo, na kuzitupa nje ya hicho kiota. Ameyakinia kwamba hawatauzoea ulimwengu. Hiyo ni kweli.

<sup>139</sup> Hivyo ndivyo Mungu afanyavyo, wakati mwingine. Loo, mnawazia kuhusu kila kitu kikubwa na kila kitu cha majigambo, na kila kitu. Msiyatazamia hayo. Mbona, mko maili milioni moja kutoka pentekoste. Wapentekoste hawakutazamia mambo ya rahisi. Waliuza waliyokuwa nayo na kuwapa maskini, kisha wakatoka pamoja na Kristo, pekee. Halafu, siku hizi, inatupasa kumiliki mlolongo wa Makadilaki kabla hatujawa wa kiroho. Imekuwaje? Kuna kasoro, mahali fulani.

<sup>140</sup> Mimi, hebu nishike njia pamoja na wachache wa Bwana waliodharauliwa. Nimeanza na Yesu. Bwana, nipitishe, chini ya hali yoyote ya mambo.

<sup>141</sup> Watu wanaogopa Kuzaliwa upya. Hiyo ndiyo shida. Wanaogopa kuzaliwa mara ya pili.

<sup>142</sup> Mtu yeyote anajua kuwa kuzaliwa kwokwote, sijali kuko wapi, ni mchafuko. Kama kuko kwenye zizi la nguruwe, au kama kuko kwenye kibanda cha majani makavu, au kama kuko kwenye chumba cha hospitalini kilichopambwa cha waridi, kuzaliwa ni mchafuko. Wala watu hawataki kuchafuliwa.

<sup>143</sup> Lakini, nakwambia, sitaki kukutana na Mungu kwa upande wangu. Nataka kukutana na Kuzaliwa upya kwenye kiwango cha Mungu. Sijali kama inanilazimu kulia, kulia kwa uchungu, kunena kwa lugha, chochote kinachonibidi kufanya. Sijali ni majirani wangapi wananisengeny. Acha nizaliwe mara ya pili.

<sup>144</sup> Sijali itakuwa na masharti gani, endapo itanibidi kuharibu sifa zote. Sina zozote, kwa vyovyote vile. Hicho ni kitu kimoja ambacho haikunibidi kuacha. Sikuwa na heshima wala sifa. Nilikuwa mshamba tu, kwanza kabisa, kwa hiyo sikuwa na kitu. Ila si—si—sijali ni nini, niko tayari kupoteza kila kitu na kuwa mjinga kwa ajli ya Ufalme wa Mungu. Mnataka kuniita, “Mtakatifu anayejibingirisha, au mwana-mizimu, au ibilisi, au msoma akili.” Sijali wanachosema.

<sup>145</sup> Ninamtaka Yesu. Hilo ndilo kusudi letu kuu. Kwamba liko kwenye kiwango gani, sijali mimi. Nataka kukutana na Yeye katika kiwango Chake; sio juu ya, kile nadhani ni sawa, wala kile mtu fulani anasema ni sawa. Ninataka juu ya kile Mungu anachosema ni sawa. Hicho ndicho. Kama Yeye alisema, “Ni yeye yule jana, leo, na hata milele,” ninataka kumwona kwenye kiwango hicho. Ikinibidi kuhubiria lundo la nguzo, na kula biskuti za magadi, na kunywa maji ya umande, ningali ninaitaka Injili. Namtaka Kristo kwenye kiwango ambacho Kristo angekuja.

<sup>146</sup> Anaingia mle ndani na kutupa wororo huo wote nje. Kila wakati hao tai wadogo wanapoanza kuketi chini, wanakalia mwiba. Kidogo unachoma. Yeye . . .

<sup>147</sup> Hivyo ndivyo. Hebu ibilisi, maadamu wao wako karibu . . . “Loo, uliokoka jana usiku?”

“Naam. Uh-huh. Naam. Niliokoka.”

“Hilo ni . . . Loo, nina furaha sana kwa jambo hilo.”

<sup>148</sup> Lakini, ukianza kuyaishi hayo maisha, mara wanasema, “Mtakatifu anayejibingirisha! *Nanii wa nanii!* Loo, ninaona uko pamoja na kundi gani.” Unaona?

<sup>149</sup> Anakuacha uhomwe, mara moja moja. Yeye hakutaki uuzoe ulimwengu huu, unaona. Anakutaka upate . . .

<sup>150</sup> Mama huyo hataki hao vifaranga vya kuku . . . hao tai kuwa kuku kamwe. Anawataka watoke kwenye kiota hicho. Haidhuru kama wako kwenye mwamba, ama mahali walipo, ana kitu bora zaidi kwa ajili yao.

151 Mungu ana kitu bora zaidi kwa Kanisa. Usiridhike tu, “Mimi ni Mpentekoste.”

152 Mtu fulani alisema, wakati mmoja, kasema, “Ndugu Branham...” Mzee kule Arkansas, alikuwa ameponywa. Alikuwa akizunguka kote kesho yake na magongo yake. Alikuwa akiuza penseli mtaani, kwa miaka na miaka. Akitembea kote, bango kubwa la matangazo, “Siyahitaji tena, tangu Yesu aliponijia,” akizunguka. Basi usiku huo, alikuwa amesimama kwenye kusanyiko, na karibu kama *hili*, katika Ukumbi wa Ukumbusho wa Robinson huko Little Rock. Naye akasema, “Hebu kidogo, Ndugu Branham,” (wakati nilipokuwa nikihubiri). Akasema, “Hebu kidogo.” Kasema, “Unajua, unapohubiri...” Alikuwa Mnazarayo. Akasema, “Unajua, unahubiri kama tu Mnazarayo. Halafu nikaona watu wengi sana hapa ni Wapentekoste. Na sasa mtu fulani ananiambia wewe ni Mbaptisti. Sielewi.”

153 “Loo,” Nikasema, “hiyo ni rahisi. Mimi ni Mpentekoste Mnazarayo wa Kibaptisti.” Jambo ndilo hilo hasa. Naam, bwana. Loo, ndugu, hizo chapa!

154 Nilikuwa nikiketi pale, tulipokuwa tukiwapandisha ng’ombe huko milimani, huku goti langu limekingama tandiko la kale la pembe kule, nikimtazama huyo mlinzi akiwaangalia hao ng’ombe wakipita. Yetu ilikuwa ni Tripod. Wa Grime, huko juu, ilikuwa ni Diamond T-Bar. Wengi wa hao wenye kanda mbalimbali na chapa mbalimbali walipita. Yule mlinzi hakujali hiyo chapa sana. Aliangalia alama ya damu.

155 Amina. Hicho ndicho Mungu atakachoangalia. Yeye anaangalia alama ya Damu. Hajali una chapa gani juu yako. Kwa nini? (Hakuna kitu kingaliweza kuingia kwenye malisho hayo ila Hereford ukoo safi.) Wala hakuna kinachoweza kuingia katika malango ya Mbinguni ila aliyezaliwa mara ya pili, kupitia Damu ya Yesu Kristo. Sijali ufanyacho, jinsi ulivyo msomi, au wewe ni mhubiri mzuri kiasi gani, au wewe ni mfuasi mzuri jinsi gani wa kanisa. Usipozaliwa mara ya pili kupitia Damu ya Yesu Kristo, ukiwa na alama ya Damu juu yako, kamwe hutaingia. Ni hayo tu. “Nitakapoiona ile Damu, nitapita juu yenu.” Ni hayo tu. Atakuruhusu uingie kibandiko cha Damu kikiwa ni sawa. Mungu ataiangalia Damu ya Mwanawe juu ya Kanisa.

156 Maskini huyu mama tai, anawaangalia hao tai wadogo, loo, kila wakati. Hawawezi kuketi. Ni kila mahali tu. Ni miiba, miiba, miiba mitupu.

157 Sasa, kuna jambo lingine linalopaswa kufanywa kwa Kanisa hilo la Pentekoste katika kiota hicho, wasiwe wasioweza kuondoka kwenye kiota. Hiyo ni sawa. Sasa, siyapigi mateke madhehebu. Sasa usiingize hilo niani mwako. Lakini, ninajaribu kusema, usiruhusu hapo pawe ndipo mahali pa kusimamia. Uko sawa. Nayapenda hayo madhehebu. Mimi ni mfuasi wa kila moja

yao. Mnaona? Hakika, nayapenda. Naam, bwana. Nilizaliwa mle. Kila mmoja yuko kanisani; nilizaliwa mle ndani. Lakini usisimamie hapo tu, usisimame tu kwenye dhehebu hilo. Endelea moja kwa moja na Mungu, mpaka—mpaka utoke huko kwa mruko wa kibinafsi.

<sup>158</sup> Sasa, muda si muda mwajua, wakati maskini huyo mama ameamua atawapa watoto wake mazoezi kidogo. Sasa, watajiunga na kanisa na kila kitu ni sawa, lakini kunaanza kunata. Kuna kasoro fulani. Ndipo maskini huyo mama atakuja pale mbele ya kiota, siku moja. Anawakagua hao jamaa wadogo, na kuna manyoya mengi yaliyolegea juu yao. Anajua kama akiwapeleka hao jamaa wadogo juu hewani, wakiwa na manyoya hayo yaliyolegea, wataavunja shingo yao.

<sup>159</sup> Nami nawaambia, iwapo kanisa la Pentekoste halitasafishwa vizuri, wataavunja shingo yao, pia. Kumbukeni tu hilo. Kuna manyoya mengi mno yaliyolegea. Hiyo ndiyo shida.

<sup>160</sup> Unajua anachofanya? Anapanda kwenye hicho kiota, na kuchukua mbawa zake kubwa na kuanza kuwapepea namna *hiyo*. Loo, kamwe hukusimama nyuma ya ndege hapo awali, hata, unakuta, manyoya yaliyolegea yanarushwa kila upande wakati upepo huo wa nguvu unaoenda kasi unapoanza kupitia kwenye hayo manyoya ya jamaa hao wadogo.

<sup>161</sup> Nawaambia, kanisa linahitaji kutikiswa kwa kiota leo, kwa Upepo wa nguvu unaoenda kasi, kuuondoa ulimwengu wote katika kanisa la Kipentekoste, ambapo wanaweza kuruka peke yao. Tunahitaji uamsho mwingine wa Injili ya kale, wa Roho Mtakatifu, uliotumwa, uliozaliwa na Mungu. Hiyo ni kweli kabisa. Hatuhitaji rais mpya; tunaye mmoja, mtu mzuri. Hatuninii wapya, hatuhitaji mameya wapya wa jiji, wowote wale. Hilo silo. . . Hiyo ni kazi yao. Lakini tunachohitaji, kama wahudumu, ni kuihubiri Injili na kulirudisha kanisa kwenye pentekoste tena, kulirudisha kwenye ujuzi wa tai tena. Hilo ndilo kanisa linahitaji. Hilo ni, loo, ninii tu. . . Hamtaki kuwa kuku. Ninyi ni tai. Hamna budi kula Chakula cha tai.

<sup>162</sup> Naye huyu hapa, ameketi pale, akiyang'oa maskini manyoya hayo madogo yote. Maana, asipoyang'oa, wao. . . yasipong'olewa, hawana manyoya ya kutosha yaliyosalia kuruka. Yeye hatawachukua mpaka maskini hayo manyoya yote madogo ya kitoto yapulizwe yawaondokee.

<sup>163</sup> Ndipo anakuja hapo juu, naye anapaza sauti. Yuko tayari kuwapa mazoezi basi. Anatokeza mbawa zake kubwa mno za futi kumi na nne namna hiyo. Hao tai wadogo wanayashika, wanapanda juu. Anazungumza nao basi, kwa sababu wameisikia sauti yake. Wanajua kumtumaini, jinsi ya kuruka. Anasema—anasema, “Sasa, watoto, nitawapeleka mkaruke peke yenu.” Kila mmoja anapanda juu, na kuweka mguu wake mdogo, na kushika ndani ya ubawa, anauma mmoja wa hayo manyoya.

Mbona, hauwezi kung’oka. Utawashikilia tai hamsini, kwa kuwa nguvu za unyoya huo ziko katika ubawa wake. Naye anashikilia kwenye huo unyoya namna *hiyo*, naye maskini mama huyo anainua mbawa zake namna *hiyo*, anaruka kutoka kwenye huo mwamba.

<sup>164</sup> Huyu hapa anaenda, akipaa juu, juu, juu, juu, mpaka anafika huko juu sana kwenye bluu, juu kabisa. Hao jamaa wadogo walikuwa hawajawahi kufika huko hapo kabla. Loo, wanakuwa tu na wakati mzuri sana.

<sup>165</sup> Muda si muda, mwajua, mnajua anachofanya? Anapinduka moja kwa moja na kuwatikisa, kila mmoja, anawatoa. Wao ni tai. Wanapaswa kujua jinsi ya kuruka. Hiyo ni kweli kabisa. Anawatikisa na kuwatoa, wawe peke yao. Vema, baadhi ya hao jamaa wadogo... Anapaza sauti, “Sawa, watoto, ninyi ni tai. Rukeni.”

<sup>166</sup> Maadamu unasema, “Vema, mimi ni mfuasi wa kanisa *hili*. Nawaambia. Sijui kuhusu *Hilo*.” Kamwe hutaruka. Uh-huh. Uh-huh. Vema. Unahitaji kutikiswa wakati mmoja, juu hewani.

<sup>167</sup> Hao tai wadogo wanaanza kuruka. Anapaza sauti, “Pigepigeni mbawa zenu, enyi watoto. Endeeleni tu kupigapiga imani yenu ndogo, juu chini. Mko juu vya kutosha sasa hamtaigusa ardhi.” Mnajua nini? Halafu anachofanya, anaruka ghafla upande mmoja, awaangalie. Anaelea papo hapo karibu. Nao hawa hapa, ka—kama tu uamsho wa Kipentekoste hasa, wikipinduka juu chini, mmoja juu ya mwingine, huyo mwingine, wikipigapiga, kwa yote wawezayo kutenda. Hawajali. Wana imani kuu mno kwa mama yao aliye nje kule akiwaangalia.

<sup>168</sup> Kanisa linapaswa kufanyaje? Kama mmoja wao hao wadogo, tai akitetereka, yeye anashuka chini na mbawa hizo kubwa na kumtwaa, na kumwinua juu katika neema tena. Sasa, hilo si fundisho la Kibaptisti. Hiyo ni Biblia. Kwa hiyo, anamrudisha moja kwa moja juu tena. Anamtikisa tena; anamwacha aanze upya. Amina.

<sup>169</sup> Hao tai wana imani na mama yao, imani kuu mno, kwamba mama huyo atawasaidia na kuwainua juu tena. Kuwabeba juu ya mabawa ya tai, na kuwapeleka huko juu na kuwaachilia tena. Anamwacha aanze tena. Kama wewe...

<sup>170</sup> “Kama nikianguka ama nikishindwa, jalia niinuke na kujaribu tena, Ee Bwana.” Nenda tena. Mungu atakuinua urudi tena, atakupeleka huko juu na kukutikisa akuachilie tena. Jaribu kujisawazisha, na ukaze mwendo. Endelea tu kupigapiga mpaka ujue kuruka. Loo, jamani! Maskini kuku wa kale hajui lolote kuhusu hilo. Hajui kitu kuhusu hilo, kwa sababu hajawahi kwenda huko juu; hakuna hata mmoja wa wahenga wake huko juu. Yote ajuayo ni kujiunga na kanisa na kuketi chini, unaona, kwenye kitalu. Hajui mengi juu yake.

<sup>171</sup> Wakati mmoja mtu mmoja alikuwa akimwatamisha kuku, wala hakuweza kupata mayai ya kutosha. Kwa hiyo akapata kiota cha tai, akapanda juu na kuchukua yai la tai na kuliweka chini ya huyo kuku. Basi wakati lundo hilo la vifaranga lilipoanguliwa, maskini tai huyo alikuwa ni jamaa mdogo mwenye sura ya kuchekesha, kwa hao kuku wengine.

<sup>172</sup> Hivyo ni karibu tu jinsi inavyokuja, mmoja kutoka kwa kila kikao. Ni karibu tu jinsi inavyotukia. Hiyo ni kweli. Naye huyu hapa, maskini jamaa mwenye sura ya kuchekesha.

<sup>173</sup> Asingeweza kuelewa kilio cha huyo kuku, maskini yule kuku huko nje kwenye—kwenye lundo la samadi katika kitalu, “Tutakuwa na mlo wa umma usiku wa leo. Tutafanya *haya* yote, namna hiyo. Chwi, chwi, chwi. Siku za miujiza zimepita. Hakuna kitu kama uponyaji wa Kiungu. Chwi, chwi, chwi, chwi.” Wakila takataka hiyo ya karamu za kale za karata, na michezo, na kuvua nguo, na kila kitu namna hiyo, televisheni na upuuzi huo wote wa namna hiyo.

<sup>174</sup> Maskini jamaa huyo alikuwa ni tai. Hicho hakikumkaa. Kilimfanya atapike, kukinusa. Angeninii, “Jamani, kamwe sitawezana na hicho.” Akitembea kote, jamani, alionekana jamaa mdogo wa kuchekesha.

<sup>175</sup> Wakasema, “Loo, njoo huku, kipenzi. Tutakuwa na karamu kubwa mno, usiku wa leo. Tutatumika.”

<sup>176</sup> Hakutaka wowote wa upuuzi huo. Alitembea kote na kuona. “Kitu gani? Mimi ni bata mwenye sura ya kipekee hapa.”

<sup>177</sup> Basi nakwambia jambo moja, ndugu, mtu anapozaliwa kuwa mwana wa Mungu, kanuni za imani za kale kamwe hazitamridhisha. La, bwana. Mambo ya ulimwengu, michezo ya mipira ya vikapu, na karamu, na—na michezo ya karata, na namna hizi zote za burudani ambazo makanisa ya kisasa hufanya katika siku zetu. Si ajabu, wanakubali, “Mungu yuko wapi?” Wamemhuzunisha Mungu akawaondokea. Hiyo ni kweli kabisa. Naam, bwana. Kuku wanapenda takataka ya namna hiyo, lakini tai hawaipendi. Hiyo si chakula cha tai.

<sup>178</sup> Huyu hapa akatembea, kule. Na, jamani, ninii yote. . . wote wakatazama pande zote. Wote walikuwa wamekimbilia mahali *hapa*. Ninii tu. . . Angechakura baadhi ya vitu vyenye sura chafu mno, nao wangekimbia pale na kula. Uh! “Loo, hima, hima, ukajiunge nasi.”

<sup>179</sup> Lakini yeye ni mtu aliyetengwa. Naam, bwana. Hakutaka hata mmoja wa upuuzi huo. Haikuonekana sawa kwake. Hakikunukia vizuri. Hakuwa na mazingira yanayofaa pale. Hakupenda hicho, hata kidogo. Alisema, “La, la.”

<sup>180</sup> Basi siku moja, maskini yule mama tai alikuja kumtafuta. (Nina furaha sana kwamba Yeye alikuja kunitafuta.) Akaruka juu ya hicho kitalu, akaangalia huko chini, ndipo akamwona



kifaranga wake. Ndipo akapiga makelele. Akasema, “Kipenzi, wewe si kuku. Wewe ni wangu.” Wakati alipoisikia sauti hiyo, aliangalia juu. Hiyo ilisikika nzuri. Asili yake ilikuwa ni tai. Asili yake.

“Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele.”

“Amina,” akamjibu kwa sauti kuu.

<sup>181</sup> “Usiupende ulimwengu wala mambo yaliyo katika ulimwengu; ukifanya hivyo, kumpenda Mungu hakumo ndani yako.”

“Amina,” akasema. “Hiyo inasikika nzuri.”

<sup>182</sup> “Nikirudi huko, kipenzi, unaweza kuruka. Kitu pekee unachopaswa kufanya ni kupigapiga mabawa yako madogo ya imani. Yatakubeba.”

“Nitaondokaje kwake, mama?”

<sup>183</sup> “Pigapiga tu mabawa yako. Hivyo tu. Utatoka moja kwa moja. Chukua tu imani yako na upige hatua moja kwa moja nayo. Anza kuondoka, kwa sababu wewe ni tai, kwanza kabisa. Hakika. Wewe ni tai, kwanza kabisa. Pigapiga mabawa yako.” Alikuwa akielea kote, huko juu. “Unaonekana kama mmoja wangu huko chini, mahali ulipo.”

<sup>184</sup> Ndipo yule jamaa mdogo akaruka kwa miguu yake, akaruka-ruka, mara nne au tano, unajua, kama vile anavyopiga makofi yake madogo, au mabawa, pamoja, namna hiyo. Na muda si muda mwajua, akaondoa miguu yake ardhini.

<sup>185</sup> Lakini mnajua alilofanya? Maskini tai huyu, aliketi moja kwa moja juu ya nguzo moja kwenye kitalu, moja kwa moja katikati ya dhehebu kubwa la Kipentekoste. Mnajua nini? Mama tai akaruka huko tena. Akamtazama, amevaa dangirizi, amekata nywele, amejipodaa uso. Kasema, “Kipenzi, unaonekana zaidi kama mwewe wa kipentekoste kuliko unavyoonekana kama tai wa kipentekoste. Itabidi ujioshe zaidi ya hivyo, la sivyo siwezi hata kukuchukua.” Kweli.

<sup>186</sup> Simaanishi kuudhi hisia zenu, lakini nataka kuwanyoa kitu fulani. Hebu nikwambie, ndugu. Mbona, kanisa la Pentekoste linahitaji utakaso, tangu mimbarani hadi kwenye marefu ya kanisa, hiyo ni kweli kabisa, kuweka kando mizigo. Si ajabu hatuwezi kuwa na uamsho, tukila vitu vya koho, kukaa nyumbani usiku ukiangalia televisheni uipendayo badala ya kwenda kwenye ibada ya mkutano wako wa maombi. Kuvaa maskini hizi. . . Wanawake wakivaa nguo hizi, nao wanaume wanakunywa pombe kidogo, na kufanya mizaha michafu na kadhalika wenyewe kwa wenyewe. Mnamaanisha nini, wanaume? Mungu kamwe hawezi kushuka kwenye machafuko ya upuuzi kama huo.

<sup>187</sup> Mnaweza mkawa na makanisa yaliyo makubwa kuliko yote nchini. Mnaweza kuwa na pesa nyingi zaidi ya mlizowahi kuwa

nazo. Hiyo haina uhusiano wowote nalo. Mnaweza kushirikiana na wale mnaowaita umati bora wa wasomi. Huenda ukavaa suti bora zaidi, lakini, ndugu, Mungu anataka moyo safi na mikono safi. Anataka kanisa lililosafishwa, ndipo anaweza kujionyesha Mwenyewe.

<sup>188</sup> Wakati Mungu anapotandaza mbawa Zake kubwa na kuonyesha nguvu Zake, kwamba Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele, tai akisema, “Naam, Bwana. Hilo ndilo ninalotaka. Ninalipigania. Ninakuja kwake.” Hakika. Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele.

<sup>189</sup> Jamani, wakati wetu ulienda wapi? Na—najisikia tu kuhubiri sasa. Ninaninii tu. . . Lakini—lakini sisi. . . Wapi?

<sup>190</sup> Loo! Kile kanisa la Pentekoste linachohitaji ni kusafishwa. Linahitaji kuoshwa. Linahitaji kusuguliwa, utakaso. Enyi watu, ninyi si wa ulimwengu. Msijifaninishie kama watu wengine. Msijaribu kujifaninisha na bingwa fulani wa sinema. Wewe ni binti ya Mungu. Wewe ni mwana wa Mungu. Usijaribu kuwa Matt Dillion au mtu fulani. Usijaribu kuwa Peabody Ernie, au lolote lililo jina lake, au baadhi ya wanaume hao. Wewe si. . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] “Usiyapende mambo ya ulimwengu. Mkiupenda ulimwengu, au mambo yaliyo katika ulimwengu, kumpenda Mungu hata hakumo ndani yenu.” Najua, ndugu, hiyo inachefua. Hiyo inakuchefua.

<sup>191</sup> Maskini mama yangu wa kusini alizoea kuniambia hivyo. Sisi sote watoto wadogo tungekuja Jumamosi usiku, na birika kubwa la kale la mwerezi, naye angemwaga maji ndani yake, na—na kumwosha mtoto mdogo. Nami nilikuwa ndiye wa mwisho kati ya kumi. Nami nilikuwa wa mwisho kuoga katika birika lile lile la maji, tunayapasha tu moto kidogo. Halafu basi mama angechukua. . . Tulikuwa maskini sana, sisi. . .

<sup>192</sup> Angechukua maskini ngozi za nyama na kuziyeusha kabisa, apate gri—grisi kutoka kwake. Tusingeweza kununua mafuta ya nguruwe, na kwa hivyo angetoa griisi kwake, kuitia kwenye ugali. Nasi tulikuwa na mbaazi jicho jeusi, mboga za tanipu, na ugali. Na—nasi tukapata ninii yetu. . .

<sup>193</sup> Tulikuwa na mizio na kadhalika, naye mama, kila Jumamosi usiku, angetupa kipimo cha mafuta ya mbarika. Bado si—siwezi kuvumilia kitu hicho, kukinusa. Nami ningemjia, nimeshika pua yangu. Ningesema, “Mama, acha, acha, acha. Kamwe siwezi kuyavumilia.”

<sup>194</sup> Akanipa neno zuri. Kasema, “Mwanangu, yasipokuchefua, hayakufai kitu.”

<sup>195</sup> Ndivyo ilivyo na kuhubiri, Neno hili. Lisipokuchefua, vizuri sana, kusudi lifanye ulaji bora wako wa kiroho uanze kufanya kazi, halitakufaa kitu. Hiyo ni kweli. Neno hukuweka huru, na huru kweli kweli, linakata pingu. Mnaamini hilo?

<sup>196</sup> Kanisa linahitaji uamsho wa Roho Mtakatifu. Linahitaji kusafishwa kwa nyumba. Hawa ni tai. Usiwalishe chakula cha kuku. Wao ni tai. Watoe huko nje ambako itawabidi kuruka la sivyo wafe. Hakuna lingine. Naye Mungu ataangalia urithi Wake. Yeye kamwe hayuko mbali mno. Daima yuko karibu, kukuinua. Je, mnaamini hilo?

Na tuinamishe vichwa vyetu basi kwa ajili ya maombi.

<sup>197</sup> Ni wangapi wangetaka kukumbukwa sasa? Na kusema, “Bwana, unirehemu. Nipe mawazo ya tai. Nipe shauku za tai. Nipe uhai wa tai. Jalia niruke katika bluu Yako huko ng’ambo, Bwana, ambako mambo yote yanawezekana kwa hao wanaoamini. Jenga imani ndani yangu. Jalia mabawa yangu yakue. Jalia misuli yangu, karibu na mabawa yangu, ikue hata niweze kweli kumwona Yesu.” Loo, Mungu awabariki.

<sup>198</sup> Baba wa Mbinguni, loo, huenda U—Ujumbe ulisikika wa kukosoa, Bwana, lakini haukukusudiwa hivyo. Ulikuwa tu katika maskini njia ya pekee niliyo nayo, ya kuwafanya watu wajue, Bwana, kile, ninachoamini, kwamba Wewe unajaribu kuwafikia, kulitikisa kanisa. Urithi huu mkuu Wako, kanisa hili kuu la Kipentekoste, kanisa kuu, jinsi lilivyo; Umetikisa kila namna ya karama karibu nao, kila namna ya ishara na maajabu, nao wanaketi kitako, kama kuku, wakati mwingine. Ee Mungu, jalia waone wao ni tai. Wanaweza kuruka, waichukue tu imani yao na kuruka waondoke kwake, waondokee msemu huu wa kale, “Haliwezi kutendeka. Halina kitu.” Ee Mungu, ninaomba ya kwamba utambariki kila mmoja hapa alasiri ya leo, na jalia kila mmoja wao azungukezunguke karibu chini ya mbawa za Yehova. Lijalie, Baba. Ninawakabidhi Kwako, katika Jina la Yesu, Mwanao. Amina.

<sup>199</sup> Ni juu ya Bwana Mungu, kile afanyacho. Sasa tutakuwa na mstari wa maombi, ili tuweze kutoka hapa. Nataka mwende kanisani, usiku wa leo. Mungu awabariki. Mnampenda Bwana? Amina.

<sup>200</sup> Hebu tuimbe mara moja tu zaidi, ili niweze kuusikia katika Tulsa, kundi hili kubwa mno.

Nampenda, nampenda  
Kwani alinipenda kwanza  
Akanunua wokovu wangu  
Kule Kalvari.

<sup>201</sup> Vema.

Mimi . . .

Hebu tuufanye uvume sasa, Kwake. Ujumbe umeisha. Na tumwabudu tu.

...Nampenda  
 Kwani alinipenda kwanza  
 Na kununua wokovu wangu  
 Kule Kalvari...

202 Sasa hebu kwa namna fulani tuinamishe vichwa vyetu, na kuinua mikono yetu, wakati umati unapotulia sasa.

Nampenda, nampenda  
 Karibia, Bwana.

Kwani alinipenda kwanza  
 Na kununua wokovu wangu  
 Mtini Kalvari.

203 Hiyo ilikuwa ipi, mia moja ama hamsini? Hamsini? Wewe uliye na kadi ya maombi namba moja, inua mkono wako. Simama kwa miguu yako ukiweza. Kadi ya maombi namba moja, H. H, namba moja, inua mkono wako. Kadi ya maombi namba moja, simama. Je, wewe ndiye—je, wewe ndiye mtu huyo, mama? H, namba moja, njoo papa hapa. H, namba mbili?

204 [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] "...kondoo waliopotea wa Israeli." Hiyo ni kweli?

205 Sasa, kuna makabila mangapi ya watu duniani? Makabila matatu: watu wa Hamu, Shemu, na Yafethi. Sasa, hao walikuwa ni Myahudi, Mmataifa, na Msamaria, ambaye ni nusu Myahudi na Mmataifa. Mliona?

206 Ni wangapi wanajua kwamba Yesu alimpa Petro zile funguo kwenye Pentekoste, awali? Hiyo ni kweli. Akafungua, kwa zile funguo za Ufalme, huko Yerusalemu, kwa Wayahudi. Hiyo ni kweli?

207 Filipo alishuka akawabatiza, huko Samaria. Kwa kuwa Roho Mtakatifu alikuwa bado hajawajilia, kwa sababu, Petro alikuwa na funguo; akashuka akaweka mikono yake juu yao, nao wakampokea Roho Mtakatifu, wale Wasamaria. Hiyo ni kweli?

208 Huko nyumbani kwa Kornelio, ni nani aliyeitwa huko juu? Petro.

209 Tangu wakati huo, hakuna kitu kingine chochote kilichosemwa juu yake. Naam. Vizazi vyote vilikuwa na... Makabila yote yalifunguliwa Injili: watu wa Hamu, Shemu, na Yafethi.

210 Sasa, kama ukiangalia, nataka uangalie. Sasa, kulikuwa na matabaka mawili ya watu, mawili ya makabila hayo, wakimtazamia Masihi. Yalikuwa ni yapi? Na walikuwa ni nani? Walikuwa ni Myahudi na Msamaria. Lakini, Mataifa, sisi, tulikuwa Waanglo-Sakson. Tulikuwa na rungu mgongoni mwetu, tukiabudu sanamu. Hatukuwa tukimtazamia Masihi yeyote.

211 Sasa, ninashikilia tu usikivu wenu, nikiweza, mpaka m—mstari wa maombi utakapokuwa tayari, kusudi wote waweze kuwa tayari kuingia kwenye mstari wao.

212 Sasa, hatukuwa tukimtazamia Masihi yeyote, kwa hivyo hatukumpokea yeyote. Kwa hivyo basi, lakini, sasa, kwa wale waliokuwa wakimtarajia Yeye, aliwatokea. Sasa, ni wangapi wanaoamini hilo?

213 Vema, sasa—sasa, wakiisha kumkataa Masihi wao, basi, kumbukeni, Yeye aliwaendea Wayahudi. Alionyesha ishara ya aina gani? Alijua siri ya moyo wao. Sasa kanisa la Kiorthodoksi lilisema nini kumhusu? “Yeye ni Beelzebuli, mpiga ramli.”

214 Yesu akasema, “Nimewasamehe hilo. Lakini siku moja Roho Mtakatifu atakuja kufanya jambo lile lile, na, kunena dhidi Yake, hakutasamehewa kamwe katika ulimwengu huu, wala katika ulimwengu ujao.” Hiyo ni kweli?

215 Sasa angalieni, alifanya ishara hiyo mbele ya Wayahudi; aliifanya kwa Wasamaria; lakini kamwe si kwa Mataifa. Huwezi kupata kisa kimoja chake. Hapana, bwana. Lakini kabla hajaondoka. . . Sasa, Yeye alimwambia yule mwanamke. . . Sasa mtazame mwanamke huyu, kahaba yule, tunavyomwita.

216 Alijua zaidi juu ya Mungu kuliko nusu ya wahubiri Marekani. Hiyo ni kweli. Wao ni werevu sana. Ha—hawana nafasi ya ujuzi wa kimbinguni. Wengi wao ni Wakristo wazuri, ndugu wa kimbinguni, bali baadhi yao wangali ni kuku.

217 Halafu, akakaribia. Na maskini mwanamke huyo. . . Akatoka nje, akawatuma wanafunzi Wake, akaketi hapa chini. Kwa sababu, Wasamaria walikuwa wakimta-. . . Ni wangapi wanaojua Wasamaria walikuwa wakimtarajia huyu, Masihi? Mnaamini hilo? Vema, hebu niwanukulie, Yohana Mtakatifu 4, sasa. “Mwanamke alikuja kisimani, mwanamke Msamaria. Akasema. . .”

218 Sasa, kabla sijasahau, kutoka arobaini hadi hamsini, katika H. Arobaini hadi hamsini, chukua nafasi yako. Vema. H, arobaini hadi hamsini, hizo ndizo kadi zote za maombi, wachukue nafasi zao.

219 Sasa angalieni, alipokwenda kisimani siku hiyo na kuketi chini, nao wanafunzi wakaenda mjini kununua vyakula. Wakati walipokuwa wameenda, mwanamke mrembo alikuja, na mtungi kichwani mwake. Naye akashusha winchi chini, kuteka maji. Ndipo akamsikia Mtu akisema, “Nipe maji ninywe.” Ndipo akaangalia, akamwona Myahudi.

220 Alikuwa na thelathini tu, lakini Maandiko yalisema alionekana ana hamsini. Ni wangapi wanaojua hilo? “Wewe ni Mtu usiyezidi umri wa miaka hamsini, Nawe wasema kwamba umemwona Ibrahimu?”

Akasema, “Ibrahimu asijakuwako, MIMI NIKO.” Hiyo ni kweli.

Kwa hiyo wakasema, “Wewe si zaidi ya miaka hamsini.”

<sup>221</sup> Naye huyo hapo, ameketi pale kisimani. Huyo hapo Yesu, ameketi katika mandhari ya kitu kama hiki. Akasema, “Nipe maji ninywe.” Walikuwa na ubaguzi wakati huo, kama waliokuwa nao huko Kusini, watu weusi na wazungu. Akasema . . .

<sup>222</sup> “Si desturi Kwako, ukiwa Myahudi, kuniomba mimi, mwanamke, Samaria,” kasema.

<sup>223</sup> Akasema, “Mwanamke . . .” Sikilizeni sasa, ninalowaambia. Mtalikosa. “Mwanamke, kama ulijua ni Nani uliyekuwa ukizungumza naye, kama ungalijua, ungeniomba Mimi maji unywe. Nami ningekupa maji usije hapa kuchota.”

Mwanamke akasema, “Kisima ni kirefu. Wewe huna kitu cha kuchotea.”

<sup>224</sup> Ndipo basi mazungumzo yakaendelea. Alikuwa akifanya nini? Akiwasiliana na roho yake. Hilo ndilo jambo lile lile ninalofanya sasa hivi, kujaribu kushikilia usikivu wako.

Yeye akasema, “Nipe maji ninywe.”

<sup>225</sup> Mazungumzo yakaendelea mpaka akapata shida yake ilikuwa ni nini. Ni wangapi wanaojua ilikuwa ni nini? Alikuwa akiishi katika uzinzi. Kwa hiyo akasema, “Mwanamke, nenda kamwite mume wako uje naye hapa.”

Akasema, “Sina mume yeyote.”

<sup>226</sup> Kasema, “Hiyo ni kweli. Umekuwa na watano, na yule unayeishi naye siye mume wako.”

<sup>227</sup> Sasa, je, huyo mwanamke . . .chini ya hali yake, akiwa kama vile tunavyofikiria. Yeye, kahaba, mwanamke mwenye sifa mbaya, sikilizeni yale aliyojua kuyahusu Maandiko. Kamwe hakumwita kama wahubiri walivyomwita, “Beelizebuli, mpiga ramli, ibilisi.”

<sup>228</sup> Na mtu yeyote anajua kuwa kupiga ramli ni kwa ibilisi. Kwa hiyo mpiga ramli ni nani? Ni mtu aliyepotoka.

<sup>229</sup> Ibilisi hawezi kuumba kitu. Yeye ni, kama yeye ni muumbaji, angeweza kujifanyia ulimwengu. Lakini anaweza kupotosha kile ambacho Mungu ameumba. Mnalipata hilo? Hapa, hapa, linasikika chapwa, katika kusanyiko lililochanganyika. Mtu anaweza kuoa mke na kuishi naye kama mke, nayo hayo malazi ni safi. Tendo lile lile na mwanamke mwingine, yeye amepotea, mnaona, ni kupotosha kitu kilicho sawa. Mnaelewa ninalomaanisha? Shetani hupotosha.

<sup>230</sup> Mpiga ramli ni mwanaji mpotovu wa Mungu, aliyepotoshwa katika milki za ibilisi.

<sup>231</sup> Halafu, angalieni, yeye hakumwita hivyo. Alisema, “Bwana, naona ya kuwa Wewe ni Nabii.” Ni wangapi wanaojua yeye alisema hivyo? Tofauti kabisa na hao wahubiri walivyosema. Kasema, “Naona—naona ya kuwa Wewe ni Nabii.”

<sup>232</sup> Sasa angalieni. Sikilizeni. “Tunajua. Sisi Wasamaria, tumefundishwa. Tunajua, ajapo Masihi, Yeye atafanya mambo haya.” Je, hiyo ilikuwa ndiyo ishara ya Masihi? Ndivyo? “Tunajua, kwamba ajapo Masihi, Yeye atafanya mambo haya. Lakini U nani Wewe?”

Yesu akasema, “Mimi ninayesema nawe Ndiye.”

<sup>233</sup> Akakimbia mjini, na kuwaambia hao wanaume, “Njoni, mwone Mtu aliyeniambia mambo niliyoyatenda. Je, haimkini huyu kuwa ndiye Masihi?”

<sup>234</sup> Lakini kamwe hakufanya hivyo kwa Mataifa. Lakini je, Yeye aliwaahidi Wamataifa? Mbona, tuna miaka elfu mbili ya mafunzo, kama vile tu Wayahudi na Wasamaria walivyokuwa nayo, ya mafunzo, wakimtazamia Masihi.

<sup>235</sup> Sasa, Yesu alisema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Lutu, huko Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika Kuja kwake Mwana wa Adamu.”

<sup>236</sup> Sasa angalieni. Katika siku za Sodoma, walikuwa na uamsho pamoja na wasomi, pamoja na Lutu. Billy Graham mamboleo alishuka kule na kuihubiri Injili, akawapofusha. Lakini angalia kile. . .

<sup>237</sup> Ibrahimu alikuwa ndiye Kanisa, teule, la kipentekoste, lililoitwa litoke, likatengwa na mambo ya ulimwengu.

<sup>238</sup> Sasa, kunao wapentekoste katika kanisa la Methodist. Kunao wapentekoste katika kanisa la Baptisti. Wapentekoste sio dhehebu. Ni tukio ambalo mtu yeyote anaweza kupata, anayeitaka. Pentekoste ya kimadhehebu haina haki juu ya Baraka yoyote ya kipentekoste, kama Mkatoliki anaweza kuipata. Wewe ni mpentekoste kwa sababu una Baraka ya kipentekoste moyoni mwako.

<sup>239</sup> Kwa hivyo, Ibrahimu ndiye aliyeitwa atoke, naye Malaika huyu alikuwa ameketi huko juu pamoja na Ibrahimu. Na baada ya Malaika kuondoka. . . Yeye alimwita, “Bwana.” Elohimu. Ni wangapi wanaojua kwamba Elohimu alikuwa ndiye Yehova Mungu mkuu? Hakika. Bwana Mungu, na Yeye akaketi huku ameelekeza mgongo Wake kwenye hema. Angalia kile alichomwambia Ibrahimu. Sasa, Yeye ni mgeni, hajawahi kuwa huko hapo awali. Akasema, “Ibrahimu, yu wapi Sara, mkeo?”

<sup>240</sup> Alijuaje kwamba alikuwa na mke? Na alijuaje jina lake lilikuwa Sara? Sasa, Biblia ilisema ya kwamba Ibrahimu alimwambia ya kwamba alikuwa hemani, nyuma Yake; hemani, nyuma Yake.

241 Alisema, “Ibrahimu, nitakurudia kulingana na wakati wa uhai, ambapo nilikuahidi mtoto huyu. Nitakupa.” Naye Sara, sio kwa sauti kubwa, lakini alicheka kimoyomoyo.

242 Ndipo huyo Malaika, huku ameuuelekeza mgongo Wake kwenye hema, akasema, “Kwa nini Sara akacheka?” Mnaona hiyo? Yesu alisema hilo litatukia miongoni mwa Mataifa, kabla tu ya wakati wa mwisho, Masihi angeshuka chini katika mfano wa Roho Mtakatifu.

243 Jambo la kwanza ambalo Masihi alianza kufanya hapo alipobatizwa katika Yordani, kwa Roho Mtakatifu, lilikuwa ni lipi, Yeye alifanya nini? Alianza kuwaponya wagonjwa.

244 Ishara Yake ya mwisho ilikuwa ni ipi, na ishara Yake kabla hajawaacha? Ishara hiyo papo hapo.

245 Uamsho wa kipentekoste ulileta nini? Kuwaponya wagonjwa, miujiza na ishara.

246 Jambo la mwisho ni lipi? Hili hapa. Ni wangapi huko nje walio wagonjwa na hawana kadi ya maombi? Inua mkono wako. Kuwa na imani na uamini. Mtu fulani anasema, “Vipi kuhusu hilo, Ndugu Branham?” Roho huyo wa Mungu, Huyo anayetoa ahadi, hawezi kushindwa na hiyo ahadi. Nyinyi msio na kadi za maombi, nawapa kisogo. Ombeni. Na ikiwa Mungu ni Mungu, ikiwa jibu Lake ni kweli, nami nimewaambia Ukweli kupitia majuma haya, kwamba hii ndiyo ishara ya kuonekana Kwake karibuni.

247 Akili yoyote iliyostaarabika, ya kawaida inajua kuwa tuko mwishoni mwa kitu fulani. Ustaarabu hauwezi kuendelea zaidi. Unajipindapinda tu na kutetemeka. Unangojea nini? Wakati wake u—umekwisha kupita zamani sana. “Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu,” uvumilivu. Umeongezewa ovataimu, kwa ajili ya Wateule. Umepita kwa mbali sana, bali Mungu anasubiri kuliweka Kanisa Lake katika utaratibu. Anakusubiri wewe na mimi.

Na azijalie hizo baraka. Nyinyi ombeni.

248 Wakati mwanamke alipogusa upindo wa vazi Lake. Baadhi yenu ninyi wanawake huko nje sasa, hebu hii iwe kama hadithi ya Biblia. Baadhi yenu ninyi wanawake mnaoamini sasa, na mnaamini kwamba mna imani ya kutosha kumwamini Mungu, aminini kwamba lolote ambalo Mungu amesema ni kweli. Basi palikuwapo na mwanamke mdogo aliye gusa upindo wa vazi Lake. Ndipo alipoligusa vazi Lake, aligeuka, akasema, “Ni nani aliyenigusa? Ni nani aliyenigusa?”

249 Ndipo wote wakakana. Kasema, “Vema, kila mtu anakugusa.” Petro akamkemea, akasema, “Kila mtu anakugusa. Kwa nini ukasema hilo jinsi hiyo?”



250 Akasema, “Lakini naona ya kuwa nimekuwa dhaifu.” Hiyo ndiyo tafsiri sahihi. “Nguvu zimenitoka.” Na *ngu*vu ni “uweza.” Ni wangapi wanaojua hilo? “Nguvu zimenitoka.”

251 Basi akaangalia pande zote, kwenye huo umati, mpaka akampata maskini huyo mwanamke. Naye akamwambia ya kwamba kutokwa kwake na damu kumekoma, kwa kuwa imani yake ilikuwa imemponya. Hiyo ni kweli?

252 Biblia ilisema, kwamba, “Yeye sasa hivi ni Kuhani Mkuu anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu.” Ninyi, wageni, mnaamini hilo?

253 Sasa, kumbukeni, uponyaji, kama Yeye angalikuwa amesimama hapa amevaa suti hii, aliyonipa, asingewaponya. Kama ukija hapa jukwaani, “Bwana, utaniponya?” unajua yale angekwambia? “Tayari nimefanya hivyo. Nilijeruhiwa kwa makosa yako. Kwa mapigo Yangu uliponywa.” Wokovu na uponyaji ni bidhaa iliyokamilika. Ni imani yako kuukubali.

254 Sasa, Yeye angefanya jambo fulani kuthibitisha ya kwamba alikuwa Masihi. Sasa, mambo haya hayathibitishi kwamba mimi ni Masihi yeyote. Mimi ni mwenye dhambi aliyeokolewa kwa neema. Na haidhuru Mungu angenitia upako kiasi gani, hana budi kukutia upako, pia. Haitafanya kazi na mimi pekee. Inahitaji wewe, kuifanya ifanye kazi. Haijalishi ni kwa kiasi gani Roho Mtakatifu anaweza kuja juu yangu, hana budu kuwa juu yako, pia. Lakini ikiwa “Yeye ni Kuhani Mkuu anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu,” nayo Biblia ilisema, “Ni yeye yule jana, leo, na hata milele,” basi atatenda vivyo hivyo. Yeye yuko hapa, ndani yetu. Je, mnaamini hilo?

Sasa, kila mtu, kaa kwenye kiti chako, iweni na kicho, ombeni.

255 Na Bwana Mungu ayajalie hayo. Ninii tu, Bwana, tafadhali. Watu hawa wapendwa . . . Mimi . . . Bwana, unajua kusudi langu la kuwa hapa. Nami naomba ya kwamba utawajalia kuona, kama hawataona tena, wajalie kujua kwamba Kuja kwa Bwana kumekaribia. Jalia wajue kwamba hizi Jumbe, zinazoonekana kali, zinawachochea, sio kujifanya mwerevu, sio kuwa ninii yangu . . . ndani yangu. Bali kwa sababu umelipaka mafuta, na kusema hivyo. Lithibitishe, Bwana. Nimezungumza kwa niaba Yako. Nena kwa niaba yangu, Bwana, kwamba maneno yangu ni ya kweli, kwa sababu yanatoka Kwako. Ninaomba katika Jina la Yesu. Amina.

Upokee wito wako. Usiikose siku yako.

256 Ni wangapi katika mstari huu wa maombi walio wageni kwangu? Inua mkono wako, ninyi nyote mlio wageni. Ninyi nyote mlioko huko nje, wageni, inueni mikono yenu.

<sup>257</sup> Sijui mtu ila Gene Goad anayeketi hapa, Pat Tyler papo hapo. Hao ndio tu ninaowaona. Mwanangu akisimama huko nyuma, ndio tu ninaowajua.

<sup>258</sup> Mwanamke yule anayeketi pale akiyasugua macho yake, aliyevaa kofia nyekundu, akiketi pale pale. Je, unaamini ya kwamba Yesu alikusikia ulipomwomba akuponye maumivu ya kichwa? Unaamini Yeye alikusikia? Ulikuwa ukiyaombea, sivyo? Ikiwa hiyo ni kweli, simama kwa miguu yako. Ikiwa hiyo ni Kweli, inua mkono wako. Ikiwa sikujui, wala hunijui, inua mkono huo mwingine juu, mikono yote miwili. [Dada huyo anasema, “Nimekuona hapo awali.”—Mh.] Ati nini Mama? [“Nimekuwa katika miamsho, hapo awali.”] Umekuwa katika miamsho yangu, hapo awali. Lakini, namaanisha, sikujui. [“Hapana.”] Hapana. Sawa. Sawa. Sasa yamekoma. Unaweza kwenda nyumbani uwe mzima.

<sup>259</sup> Ninataka kuwauliza ninyi watu jambo fulani. Mwanamke huyo aligusa nini? Huu hapa mkono wangu, kamwe sikumbuki. . . Amekuwa katika mikutano. Sasa ungesema, “Vipi kuhusu mtu fulani kule juu kwenye roshani, chini *hapa*, labda kwenye mkutano wakati fulani hapo awali?” Kamwe singejua ulikuwa ni nani. Jambo pekee nijualo, ni kwamba unaninii tu. . . ulikuwa tu hapa kwenye mkutano. Na yule pale. Aligusa kitu Fulani. Basi ni nini. . .

<sup>260</sup> Nilisema, kitambo kidogo kilichopita, ile Nguzo ya Moto. Je, hamwioni? Ni wangapi walio na picha Yake sasa? Wanayo hapa mkutanoni. Sasa, inaonekana kama Nguzo ya Moto. Sivyo? Na sasa, maisha Yake, inazaa nini? Kitu kile kile. Sio mimi, sasa. Hiyo, inazaa nini? Kazi zile zile ilizofanya wakati ilipokuwa katika Mwana wa Mungu. Sasa iko ndani ya wana na binti za Mungu wenye mamlaka, kwa neema ya Mwana wa kweli wa Mungu.

<sup>261</sup> Papo hapo, bwana. Unataka kuishinda shida hiyo ya moyo? Unaamini ya kwamba Mungu atakuponya, unayeketi hapo hapo? Ulikuwa ukishangalia, ukishangaa, mara maskini hisia ya ajabu ikakumiminikia. Hiyo ni kweli. Sikujui wewe. Sivyo? Hunijui nami sikujui. Ikiwa hiyo ni kweli, inua mkono wako. Unaamini shida yako ya moyo imeondoka? Punga mkono wako. Vema, basi imeondoka. Unaona?

Mnaamini?

<sup>262</sup> Huyu hapa mama ameketi moja kwa moja *hapa* ndani. Hamwezi kuona Nuru hiyo juu ya mwanamke huyo? Ana ugonjwa wa kibofu nyongo. Ataukosa. (Mungu, saidia.) Binti Small, unaamini Mungu atakuponya hilo tatizo la kibofu nyongo? [Dada huyo anasema, “Amina.”—Mh.] Basi simama kwa miguu yako. Ulikuwa na imani zaidi ya vile ulivyodhania ulikuwa nayo. Simjui huyo mwanamke. Hiyo ilikuwa ni neema ya Mungu. Ikiwa hatufahamiani, punga mikono yako *hivi*,

mama. Hapo. Sikujui. Lakini kile alichokuambia, ni Kweli? Inua mkono wako. Kile alichosema? Vema. Basi kuwa na imani, kisha uende nyumbani ukapone.

Kama unaweza kuamini!

<sup>263</sup> Mama huyu anayeketi papa hapa, mwenye shida ya tumbo, ndani ya tumbo. Naam, Effie, ndiye ninayemzungumzia. Simama, Effie. Hiyo ilikuwa ndiyo shida yako? [Dada huyo anasema, “Kweli.”—Mh.] Sikujui. Ikiwa hiyo ni kweli, inua mikono yako. Sijawahi kukuona maishani mwangu. Mungu Mbinguni anajua hilo. Nenda nyumbani. Imekwisha. Mungu akubariki.

<sup>264</sup> Ukifa katika dhambi zako, haitakuwa ni kosa la Mungu. Unaweza kuwa mwaminifu sana kwa kanisa, lakini mwenye dhambi ni asiyeamini. Mwamini Mungu. Vema.

<sup>265</sup> Sasa, watu hawa hapa, huu ni mstari wa maombi, kuweka mikono juu ya wagonjwa. Je, mtaliamini, haidhuru? Sasa, hao ni watu wasio na kadi ya maombi, ulipo mstari wa upambanuzi, huko nje bila kadi ya maombi. Sasa, ninyi wengine anzeni kuamini.

<sup>266</sup> Msisogeesogee. Mnaona? Kila mmoja wenu ni roho. Mnaona? Kila mmoja wenu ni roho. Mlijua hilo? Wasingeninii, ungekufa. Kwa hivyo, ninazungumza juu ya roho yako, sio wewe. Ni roho yako.

<sup>267</sup> Njoo hapa, mama. Unaniamini mimi kuwa ni mtumishi wa Mungu? [Dada huyo anasema, “Ndiyo, bwana.”—Mh.] Hatufahamiani. [“Naam, bwana.”] Hatufahamiani. Ikiwa hiyo ni kweli, kusudi kusanyiko, huko juu rohani, lielewe, inua tu mkono wako, ikiwa hatufahamiani, hatujawahi kukutana. Hii hapa mandhari. Kwa kuwa wa kwanza mstarini alikuwa ni mwanamke, hii hapa Yohana Mtakatifu 4, mwanamume na mwanamke, wanakutana, mara ya kwanza maishani. Iwapo huyu ni Roho wa Kristo hapa kati yetu, basi atazifanya kazi za Kristo.

<sup>268</sup> Tafadhali msisogee. Sasa, mnaharibu tu ni—ninii... M—mnawadhuru wengine. Mnaona? Nina mamlaka juu ya kila mmoja wenu. Ninajaribu kuwasaidia. Iweni kimya sana na wenye kicho. Vema.

<sup>269</sup> Iwapo Bwana Mungu ataniambia jambo fulani kukuhusu wewe... Kama nikija hapa juu... Labda wewe ni mgonjwa. Huenda usiwe, lakini ikiwa—ikiwa wewe ni mgonjwa, nami nije hapa na kukuwekea tu mikono yangu, niseme, “Utapata afya, mama,” ungeweza kuamini hilo. Maana, hiyo ni—hiyo ni kweli. Lakini kama Roho Mtakatifu alisimama hapa na... .

<sup>270</sup> Vipi kama—kama huyu alikuwa ni Bwana Yesu amevaa suti hii, amesimama hapa, nawe ungesema, “Niponye. Niponye, Bwana”? Angesema, “Nimekuponya tayari.” Lakini angefanya

kitu kama alichofanya wakati alipokuwa huku hapo awali, kama vile alivyomfanya yule mwanamke kisimani, kukujulisha kuwa huyo ni Nani. Alimjulishaje? Kwa kumwambia kitu ambacho kilikuwa maishani mwake. Hiyo ni kweli, kusanyiko? Ninyi nyote ni wageni? Angesema kitu kilichokuwa maishani mwake.

<sup>271</sup> Sasa kama atasema kitu kilicho maishani mwako, kama alivyomfanyia Simoni Petro, au kama alivyomfanyia mtu fulani katika Biblia, jinsi alivyofanya, basi hiyo ingekupa imani nyingi.

<sup>272</sup> Je, ingempa kila mmoja wenu imani, kuamini?

<sup>273</sup> Sasa, hii hapa, vema, sio nyuma ya baadhi ya mapazia meusi, sio baadhi ya maskani ya ibilisi, bali papa hapa jukwaani pamoja nanyi, kutoka kwenye Maneno ya Biblia. Huenda ikawa ni mvurugo mdogo katika theolojia, lakini ni Maandiko hata hivyo. Mnaona?

<sup>274</sup> Kama ningeweza kukusaidia, wala nisikusaidie, ningekuwa mwigaji. Singestahili kusimama hapa kando ya Biblia hii, kama ningeweza kukusaidia wala nisikusaidie. Siwezi kukusaidia. Kitu pekee ninachoweza kufanya ni kukufanya utambue jambo fulani, kwamba Kristo yuko hapa kukuponya, kukupa afya iwapo unaumwa.

<sup>275</sup> Wewe ni mgonjwa. Unasumbuliwa na ugonjwa wa kike. Ni ugonjwa wa kike. Hiyo ni kweli. Iwapo hiyo ni kweli, inua mkono wako.

<sup>276</sup> Ili kwamba usininii... utajua kwamba sibahatishi. Hebu kidogo. Weka kitu fulani moyoni mwako, na ujionbee tu, moyoni mwako, kwa chochote unachotaka Mungu afanye. Naam. Una kitu moyoni mwako sasa hivi? Ni mumeo. Ni mumeo. Unaamini Mungu anaweza kuniambia kilicho shida yake? [Dada huyo anasema, "Naam, bwana."—Mh.] Ni shida fulani kwenye ubongo. Inaitwa, kama kushupaa kwa ateri katika ubongo. Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli. Ikiwa Mungu ataniambia wewe ni nani, je, itakufanya uwe na imani nyingi? Unaamini, kwa moyo wako wote? ["Naam, bwana."] Nancy Gillespie, nenda nyumbani, Yesu Kristo alikuponya pamoja na mumeo, na anawapa afya. Mpelekee lesi hiyo. Hiyo ni kweli. Sivyoy? ["Naam."] Vema. Nenda zako.

<sup>277</sup> Sasa mnamwamini Mungu? Iweni tu na imani. Msitie shaka.

<sup>278</sup> Sasa nitaliomba kanisa hili kubwa hapa kama mtaomba pamoja nami kwa ajili ya hawa watu. Huyo ni mama ya mtu fulani, baba ya mtu fulani, kipenzi cha mtu fulani, mume wa mtu fulani. Ombeni.

<sup>279</sup> Msisogee-sogee, tafadhalini. Ninyi tu... Mnauharibu tu mkutano. Tulieni kabisa na muombe. Tutaruhusiwa kuondoka katika dakika kumi iwapo tu mtaendelea—mtaendelea kuwa na kicho.

280 Njoo, mama. Kama nisiposema neno moja, na kukuombea tu, utaamini?

Bwana Yesu, ninaomba kwamba utamponya, katika Jina la Yesu.

Njoo, ndugu yangu. Amini kwa moyo wako wote.

281 Baba yetu wa Mbinguni, katika Jina la Yesu Kristo mponye. Amina.

282 Mungu akubariki, ndugu yangu. [Ndugu huyo anasema, “Mke wangu yuko hapa, ana ninii...?...”—Mh.] Vema, bwana, njoo. Hiyo haileti tofauti hata kidogo, bwana. La. Ni sawa. Najua shida yako, lakini hakuna haja ya kukwambia. Unafikiria, ingekusaidia kama ningekwambia? [“La.”] Isingekusaidia. Vema. Lakini, hata hivyo, ugonjwa wako wa moyo ulikuacha ulipotoka hapo. Kwa hiyo nenda zako tu, ukishangilia, ukisema, “Asante, Baba.”

Njoo, bwana.

283 Katika Jina la Bwana Yesu, Baba, ninaomba kwamba Wewe utamponya. Amina.

Aminini sasa.

284 Kuwa na imani sasa, dada. Njoo, kama hii yote...Tazama, kuna karibu watu elfu tatu hapa wakikuombea sasa.

Katika Jina la Yesu, na aponywe. Lijalie, Baba.

285 Njoo. Bwana, yabisi kavu itakushika, siku moja, ikiwa huna imani sasa. Unaliamini sasa? Basi nenda ukaponywe, katika Jina la Yesu Kristo.

Njoo, dada.

286 Baba Mungu, katika Jina la Bwana Yesu, mponye dada yetu. Amina.

Njoo, ukiamini sasa.

Kila mtu aamini na kuomba.

287 Baba wa Mbinguni, ninaomba kwamba utamponya, katika Jina la Yesu. Amina.

288 Njoo. Sasa, ndugu, kama tulipata maono kwa kila mtu, ingekuwa tu...wewe...Ingewabidi wanibebbe kutoka jukwaani; mnaona, ningedhoofika. Lakini ili uweze kujua, nenda zako ukale chakula chako cha jioni usiku wa leo. Kitakuwa kitamu sana. Huo ugonjwa wa tumbo umekuacha. Unaona? Nenda ukale. Vema.

Njoo, dada.

289 Ninafanya hivyo kwa kusudi fulani, kujitupa kando, marafiki. Sababu, maono...Ni wangapi wanaojua kwamba Yesu alisema, “Nguvu zimenitoka”? Mimi, sasa hivi, ni dhaifu kweli kweli.

290 Ee Baba, ninaomba kwamba utamponya dada yetu. Kwa Jina la Yesu, lijalie.

291 Njoo, dada mpendwa. Usiwe na shaka sasa. Njoo, ukiamini kwa moyo wako wote.

292 Ee Bwana, katika Jina la Kristo, mponye dada yetu. Mpe ushindi wake, Bwana.

293 Njoo, dada yangu. Biblia ilisema, “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.”

Katika Jina la Yesu, na aponywe. Amina. Lijalie.

294 Njoo, dada. Ugonjwa wako wa mgongo ulikuacha, kwa hivyo unaweza kwenda zako, ukishangilia.

295 Mnaamini? Mnaona? Kwa nini, kwa nini? Sikilizeni. Nataka kuwauliza. Sikilizeni, marafiki. Wakati watu hao wanapokuja hapa. . . Biblia, inasema, “Waweke mikono juu ya wagonjwa, nao watapona,” ni sawa tu na kuwaambia. Hamuamini Hilo? Hakika, mnaamini.

296 Angalia hapa, bwana. Je, uniamini mimi kuwa ni mtumishi Wake? Sasa, yule pale mwanamke niliyemsimamisha muda mfupi uliopita; wewe ni mwanaume. Unaamini kwamba Mungu anaweza kuniambia shida zako? [Ndugu huyo anasema, “Naam, bwana.”—Mh.] Na—na kukuponya? [“Nina mambo manne au matano mbalimbali yaliyo kasoro hapa.”] Naam, bwana. Vema, wewe, shida yako ya tumbo ni jambo moja linalokusumbua, kidogo. Hiyo ni kweli. Naam, bwana. Naam, bwana. Na tezi kibofu chako. Naam, bwana. Kwa sababu, tezi kibofu chako kinakutia wasiwasi, na huo ndio unaokufadhaisha. Hiyo ni kweli kabisa. Unafikiri mke wako anaweza kupona, pia, ikiwa utaamini? Vema. Ikiwa utaamini kwa moyo wako wote, basi mke wako anaweza kuponywa. [“Yeye ni mgonjwa.”] Naam. Wasiwasi, na kufadhaika, na udhaifu, na kadhalika. Unaamini kwa moyo wako wote sasa, atapona? Nenda zako na useme, “Asante, Bwana Yesu mpendwa,” naye atapona, pia.

297 Bwana Yesu, ninaomba kwamba utasaidia hili, Ee Bwana, na kulifanya liwe kwamba ninii yake. . . Utukufu wa Mungu utakuja juu yake, naye ataponywa. Katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

298 Sasa nenda, ukiamini, Bw. Dodd, na uamini kwa moyo wako wote, na upone. Vema.

Njoo, bwana.

299 Baba wa Mbinguni, ninaomba kwamba utamponya ndugu yetu na kumpa afya, katika Jina la Yesu.

Njoo, dada, hapa. Mwamini Yeye kwa moyo wako wote sasa.

300 Ee Mungu, Baba yetu, ninaomba kwamba Utamponya, katika Jina la Yesu.

301 Njoo, ndugu, mlete huyo mtoto. Usiwe na shaka sasa. Mlete tu moja kwa moja, kana kwamba ulikuwa ukija moja kwa moja chini ya msalaba.

Bwana, ninawabariki katika Jina la Yesu. Amina.

Njoo, dada. Njoo, ukiamini sasa kwa moyo wako wote.

Baba, katika Jina la Yesu, ninaomba ya kwamba utamponya. Amina.

302 Amini sasa na uwe na kicho sana. Amini kwa moyo wako wote.

303 Katika Jina la Bwana Yesu, jalia apone, Bwana. Amina.

304 Njoo, dada, ukiamini kwa moyo wako wote. Amini kwamba atapona sasa na atapata kuona na kadhalika.

305 Ee Bwana, ninaomba kwamba utamponya, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

306 Hivi majuzi usiku, nikimwombea mvulana mdogo, yapata umri wa miaka kumi na mitano, kumi na sita. Alipitia hapa, yule jamaa mdogo; imani kubwa. Nilimwangalia. Nikasema, “Hakika, unajua, mwanangu.” Na—na kwa hivyo akaenda zake nje, akashuka moja kwa moja pale chini. Naye huyo mvulana mdogo, aliyezaliwa kipofu, alifunguka macho, akapiga kelele tena, “Loo, Ndugu Branham, ninaweza kuona.”

307 Hapa, hapa ndani, imewekwa kamba kutoka kwa mtoto mchanga, mtoto mwenye kichwa kilichojaa maji. Kimepungua kiasi *hicho*, katika usiku mmoja, kwa kupitia hapa tu. Mambo yanatendeka. Huna budi kuamini, hata hivyo. Mnaona? Nyinyi sio kuku. Ninyi ni tai.

Njoo.

308 Katika Jina la Yesu, Bwana, jalia aponywe kwa ajili ya utukufu wa Mungu. Amina.

Njoni, mkiamini, mkiwa na imani.

309 Mnajua, kitu kingine... Mnajua ninachowazia, marafiki? Mimi, sininii, siwakemei watu, ila nataka mjue jambo moja. Tuna televisheni nyingi kupita kiasi maishani mwetu. Tunataka burudani. Hatuninii... Mungu haonyeshi vitu hivi ili kuwatumbuiza. Anawataka muutambue Uwepo Wake. Hayo mambo yanaweza kutokea kwa kila mtu, lakini karibu yanguenua; loo, nisingeumaliza huu mstari.

310 Hapa, njoo hapa, mama. Mimi na wewe hatufahamiani. Unafikiri Mungu anaweza kuniambia shida yako ni nini? [Dada huyo anasema, “Uh-huh.”—Mh.] Je, i—ingekusaidia?

311 Ingewasaidia nyote kama—kama Mungu angesema jambo fulani sasa kwa mwanamke huyu?

312 Ni sikio lako. Unaamini kwamba Mungu ataliponya? [Dada huyo anasema, “Vema, Mungu ashukuriwe! Naam.”—Mh.]

Unahofu ni kansa. Na iko katika sikio lako la kushoto. Hiyo ni kweli? [“Hiyo ni kweli.”] Vema, ilikuwa, bali haipo sasa. Sasa, angalia. Unamwamini Mungu? [“Ninamwamini.”] Ikiwa Mungu ataniambia wewe ni nani, itakusaidia? Vema, Ruby Thompson, nenda nyumbani ukapone, katika Jina la Yesu Kristo. Unaona? Kuwa na imani.

313 Njoo sasa. Usiwe na shaka. Mungu anaweza kuniambia tatizo lako. Je, unafikiri ingekusaidia? [Dada huyo anasema, “Ndiyo.”—Mh.] Basi, kisukari, ugonjwa wa moyo, nenda zako ukapone, na umwamini Mungu. Naam. [“...?...”] Huo ni uzee tu unaokujia. Sasa, nenda tu, ukiamini.

314 Ee Bwana, naomba kwamba utamponya ndugu yetu na kumpa afya. Amina. Mungu, lijalie.

Njoo, dada mpendwa.

Katika Jina la Bwana Yesu, na apone. Amina.

Kuomba baraka za Mungu, inawezaje kushindwa?

Katika Jina la Yesu Kristo, na iwe hivyo, Bwana. Amina.

Njoo, ndugu yangu.

315 Katika Jina la Yesu Kristo, ndugu yetu na aponywe. Amina.

316 Njoo, ndugu mpendwa. Mungu akubariki. Mlete mama papa hapa. Hima, dada.

Katika Jina la Yesu Kristo, na uponywe.

Njoo.

Katika Jina la Yesu Kristo, dada yetu na aponywe sasa.

317 Naam. Amini sasa. Jambo lilo hilo litatokea huko chini, ikiwa hutatilia shaka.

318 Ee Mungu, mbariki maskini ndugu huyu mpendwa. Ninaomba, Baba wa Mbinguni, kwamba utamponya na kumpa afya. Pia jalia iwe kwamba atapata kuona na kuponywa, katika Jina la Yesu. Amina.

319 Iweni na imani sasa. Msiwe na shaka. Siwezi kuponya. Yeye yuko tu hapa. Yeye ndiye mponya. Usiwe na shaka. Kuwa kama kipofu Bartimayo, endelea kuitafuta mikono yako.

320 Katika Jina la Yesu Kristo, dada huyu na aponywe. Vema.

Njoo, dada, mpendwa.

Je, mnaamini, kila mtu? Kabisa . . .

321 Jambo fulani lilitukia. Hebu kidogo. Huyu jamaa anayeketi hapo, una pumu, bwana. Hiyo ni kweli. Ulikuwa ukiomba. Ukageuka, kusema, “Hiyo si ni ajabu?” Nitakuambia jambo lingine. Walitoa karibu theluthi mbili za tumbo lako, kwa ajili ya ugonjwa wa tumbo. Hiyo ni kweli. Sivyo? Ikiwa hiyo ni kweli, pungu mkono wako. Nasi hatufahamiani. Yesu Kristo alikuponya. Imani yako ilikuponya. Nenda zako, ukishangilia.



Loo, usiwe na shaka. Amini.

<sup>322</sup> Vema, mama. Wewe... Ngoja kidogo. Sasa, huko hapa kwa ajili yako mwenyewe. Uko hapa kwa ajili ya mtu mwingine. Hiyo ni kweli. Naye ndugu yako hayupo hapa. Ndugu yako hata hayuko katika mkoa huu. Yuko St. Louis. Yuko hospitalini. Ana ugonjwa wa moyo. Naye ni, amekuwa mhudumu. Nawe uliwazia kama nikipitia hapa na kukuwekea mikono, kwamba wewe... Mimi “nisingejua” kile nilichokuwa nikizungumzia. Lakini nilijua. Kwa hivyo, wewe nenda zako, naye atapata afya, ninaamini. Vema. Kuwa na imani. Endelea tu.

<sup>323</sup> Yupo mwanamke mwingine hapa, anayewazia jambo lile lile sasa hivi, juu ya binti aliyeuawa. Bibi Weatherman... Waterman, ndivyo lilivyo. Bibi Waterman, amini kwa moyo wako wote sasa. Binti yako alichukuliwa kwa kusudi fulani. Usiwe na shaka, mwamini Mungu.

<sup>324</sup> Ee Mungu, katika Jina la Yesu Kristo, jalia a—aponywe. Amina.

Njoo, ukiamini sasa kwa moyo wako wote.

<sup>325</sup> Ee Bwana Mungu, Muumba wa mbingu na nchi, ujalie uponyaji wa mwanamke huyu, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Amini sasa.

<sup>326</sup> Sasa angalia, hakuna tiba ya dawa. Ila kuna tiba ya Kimbinguni. Hiyo ni kweli. Unaamini hilo? [Dada huyo anasema, “Hakika.”—Mh.] Atakuwa wa kawaida na mzima.

<sup>327</sup> Laana, namlaani ibilisi huyu aliyemfanyia uovu mtoto huyu. Nami naondoa laana hii juu yake, katika Jina la Yesu Kristo. Jalia awe mtoto wa kawaida. Amina.

Lazima iwe hivyo. Sawa.

Nenda zako, ukishangilia. Pona na ule chakula chako chajioni na... Vema.

Njoo, bwana. Mwamini, kwa moyo wako wote.

Katika Jina la Bwana Yesu, na aponywe. Amina.

<sup>328</sup> Hiyo iligonga maeneo mengi sana katika kusanyiko! Hebu kidogo. Hilo, ni wangapi hapa walio na tumbo jepesi, hata hivyo? Inua mkono wako. Ni wengi sana, siwezi... Mnaona hapo? Kila mmoja wenu, mwenye tumbo jepesi, simama kwa miguu yako. Hii ndiyo njia ya kuuondoa. Simama kwa miguu yako, kwa dakika moja tu.

Simama kimya, bwana. Nenda, ukiamini, ndugu yangu.

Katika Jina la Yesu Kristo, na uponywe.

<sup>329</sup> Njoo sasa. Amini kwa moyo wako wote. Unaamini, dada? Katika Jina la Yesu Kristo, na uponywe.

330 Wasiwasi, umekuwa hivyo sikuzote, maishani mwako mwote.

331 Kila mtu anayesumbuliwa na ugonjwa wa wasiwasi, na figo, simama kwa miguu yako. Simama kwa miguu yako, kila mtu aliye nao.

332 Nenda, ukiamini sasa. Kuwa na imani. Unaona? Simama moja kwa moja *pale* chini.

333 Ee Bwana Mungu, ninakuomba umhurumie ndugu yetu, na umponye, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Kuwa na imani. Unaamini sasa, dada mpendwa?

334 Katika Jina la Bwana Yesu, na aponywe, Baba, kwa utukufu wa Mungu.

Kitu fulani kinatendeka.

335 Ni hao tu, Billy? [Ndugu Billy Paul anasema, “Una moja zaidi.”—Mh.] Naam. Naam.

336 Njoo hapa, bwana. Sisi hatufahamiani? [Ndugu huyo anasema, “Hakika.”—Mh.] Mungu anatufahamu sote wawili, sivyo? [“Hakika.”]

337 Loo, inatendeka tu kila mahali. Kumbukeni, enyi wahubiri, ndugu zangu, tai ndugu zangu wa thamani, nikiisha kutoka hapa, kwa majuma kadhaa, utakuta kusanyiko lako likishuhudia kwamba wamepona. Wameponywa, ila hawajui. Mnaona? Mnaona? Inatendeka tu kila mahali. Kwa nini hatungeweza kuwa na imani ya aina hii kwanza kabisa, marafiki? Hii ndiyo.

338 Unaamini kwamba Mungu anaweza kukusaidia? Unaamini Mungu anaweza kuniambia kilicho shida yako? [Ndugu huyo anasema, “Naam, bwana.”—Mh.] Una maumivu makali sana ya kichwa. Una vipindi vya kizunguzungu. Vinasababishwa na uvimbe shingoni. Hiyo ni kweli. Unaamini Mungu anajua wewe ni nani? [“Ninaamini.”] Wewe ni mhudumu. Jina lako ni Kasisi Jack Cole. Hiyo ni kweli kabisa. Nenda, amini, bwana.

339 Kila mmoja wenu, aliye na vipindi vya kizunguzungu ama anayeumwa na kichwa, simameni kwa miguu yenu. Kila mtu, mgonjwa, simama kwa miguu yako.

340 Loo, Mungu! Ingekuwaje kama tu ingetendeka! Ingekuwaje! Mnaiamini? Ni waaminio wangapi waliopo hapa, ambao wameshawishika ya kwamba kitu hiki ni Roho Mtakatifu? Inua mkono wako. Siwezi kufanya mambo hayo. Ninyi ni waaminio?

341 Wekeaneni mikono na umwamuru ibilisi amwache mtu huyo uliyemwekea mikono. Maombi yako ni sawa na yangu. Wekeaneni mikono, mmoja juu ya mwingine. Hiyo ni sawa.

Mama, *hapo* juu, kifua kikuu kilikuacha wakati huo.

342 Ugonjwa wa tezi kibofu umekuacha, ndugu. Unaweza kuweka mikono yako chini na kupiga makelele ya sifa.

<sup>343</sup> TB, iliyo na maskini yule mama anayesimama pale pale, imeondoka. Isahau. Yesu Kristo anakuponya.

Jambo ndilo hili, marafiki. Na tumpe Mungu sifa.

Ee Bwana, uko hapa.

<sup>344</sup> Namlaani ibilisi, katika kazi zake zote. Ninamlaani kila roho mchafu. Shetani, umefichuliwa. Umekemewa, katika Jina la Yesu Kristo. Ninakuamuru, kwa Mungu aliye hai, toka kwenye kusanyiko hili. Huwezi kuwafanya watie shaka, tena. Roho Mtakatifu amejifanya halisi mbele yao. Huwezi kuwafanya watie shaka, tena. Wamewekeana mikono. Yesu alisema, “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio: wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya.” Shetani, umepotea.

<sup>345</sup> Yesu, umeshinda. Wewe ni Mungu wa Mbingu. Jalia nguvu za maradhi na nguvu za ibilisi zivunjike, juu ya watu hawa, katika Jina la Yesu Kristo.



*KAMA TAI ATAHARIKISHAVYO* SWA60-0403

(As The Eagle Stirreth)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza Jumapili alasiri, tarehe 3 Aprili, 1960, katika Ukumbi wa Mikutano wa Munispaa huko Tulsa, Oklahoma, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2022 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

[www.branham.org](http://www.branham.org)

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS  
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.  
[www.branham.org](http://www.branham.org)